# UHURU
ya kijani

ISSN 0876 - 3896 Na. 0061 Alhamisi
Jumatano Oktoba 15, 2025





@uhuruonline www.uhurupublications.co.tz


# Miaka minne ya mageuzi makubwa Mkoa wa Kagera



RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan



MKUU wa Mkoa wa Kagera Mhe. Fatma Mwassa

**Mgodi wa dhahabu wa Stamigold ulivyoleta maendeleo Kagera**



**Mafanikio ya TANAPA kipindi cha miaka minne ya Samia**



**TANROADS Kagera ilivyochochea maendeleo ya miaka minne ya Rais Samia**



**Bilioni 94.7 zilivyotua Wilaya ya Biharamulo**



# Kagera inavyojivunia mageuzi ya maendeleo miaka minne ya uongozi wa Rais Dk. Samia

**Na SUPERIUS ERNEST**

MIAKA minne ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imekuwa ya neema kwa kila Mkoa, kwa matrilioni ya fedha yaliyotolewa na serikali kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Kagera ni miongoni mwa mikoa iliyopata neema ya matrilioni hayo kutekeleza miradi mbalimbali, ikiwemo sekta ya kilimo, miundombinu, elimu na mingineyo mingi.

Uchumi wa Kagera, unazalishwa katika vyanzo mbalimbali, ambapo zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wake hutegemea kilimo kukidhi mahitaji yao ya chakula kama chanzo cha mapato, mazao makuu yanayolimwa Mkoani kagera ni ndizi, kahawa, maharage, chai, alizeti, viazi na mihongo.

Shughuli nyingine za kiuchumi ni biashara inayochukua asilimia 5.3, huduma za nyumbani asilimia 4.3, uvuvi, uwindaji, ufugaji na zinazofanana asilimia 2.9, madini asilimia 1.9; uzalishaji wa asilimia 1.5 na shughuli za ujenzi asilimia 1.4.

**IDADI YA WATU**

Mkoa wa Kagera kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya 2022, una watu 2,989,299 sawa na asilimia tano ya watu wote nchini na ongezeko la takribani watu 500,000 kutoka sensa ya mwaka 2012.

Kagera ni mkoa wa sita kwa wingi wa idadi ya watu, ukitanguliwa na mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro, Tabora na Dodoma.

**MAPOKEZI YA FEDHA**

Mkoa wa Kagera kwa kipindi cha Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025 umepokea sh. trillion 1.131 ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za elimu, afya, maji, umeme, miundombinu kilimo, mifugo na uvuvi.

Sekta nyingine zilizonufaika na fedha zilizotolewa na serikali ya awamu ya sita ni sekta ya viwanda, biashara na uwekezaji na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

**MAFANIKIO KWA KILA SEKTA**

Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Rais Dk. Samia imejikita kuboresha miundombinu ya kutoa huduma za afya, weledi wa watoa huduma na upatikanaji wa dawa na vifaa tiba kwa wananchi wote wa Mkoa wa Kagera.

**MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA AFYA**

Idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya zimeongezeka kufikia 336 kwa kipindi cha Aprili, 2025, ikiwa ni ongezeko la vituo 87, ikilinganishwa na vituo 249 mwaka 2020, ulikuwa na hospitali moja ya rufaa ya Mkoa.

Huduma zinazotolewa zimeongezeka na kuboreshwa zaidi ikilinganishwa na huduma zilizokuwa zinatolewa Novemba, 2020. Hadi kufikia Aprili, mwaka huu, huduma za kibigwa zinazotolewa na Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Kagera, zimeongezeka kutoka tano hadi nane ikiwemo upasuaji wa pua, koo na masikio, mifupa na magonjwa ya ndani.

Huduma za kibigwa zinazotolewa na Hospitali ya rufaa ya Mkoa wa Kagera kwa wananchi wa mikoa jirani ni upasuaji wa jumla, wanawake na wajawazito, watoto, meno, macho, upasuaji wa pua, koo na masikio, mifupa na magonjwa ya ndani.

Idadi ya wananchi wanaopata huduma katika Hospitali ya rufaa ya Mkoa, imeongezeka kufikia wagonjwa 478,002 kufikia Aprili, mwaka huu, ikilinganishwa na wagonjwa 128,305 kipindi cha Novemba, 2020.

**Maboresho haya katika sekta ya afya, yamewezesha wananchi kupunguza umbali wa kufuata huduma kwa wastani wa kilometa 28, yamewezesha wananchi kupata huduma za kibingwa takribani nane ndani ya mkoa na upatikanaji wa vifaatiba vya kisasa kama CTC-scan, ECHO na ECG ambavyo awaliwagonjwa walilazimika kwenda Mwanza.**

Idadi ya Hospitali za wilaya zimeongezeka kutoka tatu, kuanzia Novemba, 2020 kufikia 11, kwa Aprili, mwaka huu, Idadi ya vituo vya afya imeongezeka kutoka 11 kwa kipindi cha Novemba, 2020 kufikia 29 kwa kipindi cha Aprili, mwaka huu na zahanati zimeongezeka kutoka 42 hadi 217 katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025.

Hali ya upatikanaji wa huduma za afya, dawa na vifaa tiba katika Mkoa wa Kagera ni nzuri sana. Dawa na vifaa tiba, vimeongezeka kutoa asilimia 85 hadi 93, kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, mwaka huu kimkoa. Nyumba za watumishi wa sekta ya afya zimeongezeka kutoka 318 hadi 423 kuanzia Novemba, 2020 kufikia Aprili, mwaka huu.

Idadi ya watumishi wa afya, wanaotoa hudumu katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa Wilaya za Mkoa wa Kagera wameongezeka kutoka 2,139 hadi 3,542 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, mwaka huu.

Maboresho haya katika sekta ya afya, yamewezesha wananchi kupunguza umbali wa kufuata huduma kwa wastani wa kilomita 28, yamewezesha wananchi kupata huduma za kibigwa takribani nane ndani ya Mkoa na upatikanaji wa vifaa tiba vya kisasa kama CTC-scan, ECHO na ECG ambavyo awali wagonjwa walilazimika kwenda Mwanza.

**ELIMU MSINGI NA SEKONDARI**

Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Rais Dk. Samia, imejielekeza kuboresha elimu hasa mazingira ya kufundishia na kijifunzia kwa ngazi zote za elimu Mkoani Kagera.

**ELIMU MSINGI**

Mkoa wa Kagera umepiga hatua kubwa kwa kuboresha elimu ya msingi kufikia Aprili, mwaka huu, Mkoa umepata shule za msingi 1,058 ikiwa ni ongezeko la shule 116 ikilinganishwa na shule 942 za msingi zilizokuwepo kipindi cha Novemba, 2020.

Idadi ya madarasa imeongezeka na kufikia 9,825, ikilinganishwa na madarasa 7,074 yaliyokuwepo Novemba, 2020. Hadi kufikia Aprili, mwaka huu, Mkoa wa Kagera ulikuwa na jumla ya nyumba za walimu wa shule za msingi 1,725 ikiwa ni ongezeko la nyumba za walimu 71, ikilinganishwa na nyumba za walimu 1,654 zilizokuwepo Novemba, 2020, Idadi ya walimu wa shule za msingi imeongezeka kutoka walimu 8,811 kufikia walimu 9,535.

**ELIMU SEKONDARI**

Mkoa wa Kagera umeongeza hatua kubwa katika kuboresha elimu ya sekondari. Hadi kufikia Aprili, mwaka huu Mkoa ulikuwa na shule za sekondari 292, ikiwa ni ongezeko la shule 68 ikilinganishwa na shule 224 za sekondari zilizokuwepo kufikia Novemba,



Katibu Tawala Mkoa wa Kagera Bw. Stephen Mashauri Ndaki

# Kagera inavyojivunia mageuzi ya maendeleo

2020. Idadi ya madarasa imeongezeka kufikia 4,480 kwa kipindi cha Aprili, mwaka huu ikilinganishwa na madarasa 2,522 yaliyokuwepo Novemba, 2020.

Hadi kufikia Aprili, 2025 Mkoa wa Kagera una jumla ya nyumba za walimu wa shule za sekondari 616, ikiwa ni ongezeko la nyumba za walimu 107, ikilinganishwa na nyumba za walimu 509 zilizokuwepo Novemba, 2020.

Idadi ya walimu wa shule za msingi imeongezeka kutoka walimu 3,219 kufikia walimu 4,105, Idadi ya maabara imeongezeka kutoka 346 hadi 513 kuanzia Novemba, 2020, kufikia Aprili, mwaka huu, hivyo kuongeza idadi ya mabweni kutoka 82 kufikia 163 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025

**MIUNDOMBINU YA SHULE ZA SEKONDARI**

Maboresho yaliyofanyika sekta ya elimu yamewezesha wanafunzi kusoma katika mazingira bora, umbali wa mwanafunzi kufuata huduma ya shule umepungua kwa wastani wa kilometa 14, kuboresha mazingira ya kufundishia kwa walimu, kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani na kuongeza ufaulu.

**VYUO VYA VETA**

Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Rais Dk. Samia imeendelea kuboresha mafunzo ya ufundi na ufundi stadi kwa vijana kujenga chuo cha kisasa cha VETA, kufanya mkoa huo kuwa na jumla ya vyuo vya VETA tisa, kufikia Aprili, mwaka huu ikilinganishwa na vyuo vinne vya VETA zilivyokuwepo Novemba, 2020.

**SEKTA YA MIUNDOMBINU**

Sekta ya miundombinu ni muhimu sana kwa uchumi wa Mkoa wa Kagera kwa kuwa Mkoa unapakana na nchi nne za Africa Mashariki.

**BARABARA ZINAZOSIMAMIWA NA TARURA**

Barabara za Lami kilometa 46.12 zimeongezeka kutoka kilometa 81.73 Novemba, 2020 hadi kilometa 127.85 sawa na asilimia 56.4 kipindi cha Aprili, mwaka 2025.

Barabara za Changarawe kilometa 864.8, zimeongezeka kutoka kilometa 1532.6 hadi kilometa 2397.4 sawa na asilimia 56 kuanzia Novemba 2020 hadi Aprili, 2025 .

Idadi ya Makalavati 1890 yameongezeka kutoka 3245 hadi 5135 kwa kipindi cha Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025. Aidha, Idadi ya Madaraja 13 yameongezeka kutoka 11 hadi 24 kwa Novemba, 2020 hadi Aprili, mwaka huu.

**MIRADI INAYOENDELEA KUTEKELEZWA MKOA WA KAGERA**

Jumla ya miradi 43 inatekelezwa Mkoani Kagera ikiwa ni matengenezo ya muda maalum, matengenzo ya kawaida, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, sehemu korofi na ujenzi wa barabara kiwango cha changarawe.

Utekelezaji wa miradi hiyo, upo hatua mbalimbali za utekelezaji kwa wastani wa chini ni asilimia 10 na wastani wa juu ni asilimia 95.

Utekelezaji wa miradi ya barabara zinayosimiwa na TARURA Mkoa Kagera, umewezesha barabara kupitika kwa asilimia 85 kwa mwaka mzima na kupunguza changamoto ya usafiri na usafirishaji wa mazao kwenda sokoni na mali ghafi nyingine.

**BARABARA ZINAZOSIMAMIWA NA TANROAD**

Serikali ya Awamu ya Sita, kupitia Walaka wa Barabara (TANROAD) umetekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara na madaraja. Ujenzi wa barabara za lami umeongezeka kwa kilometa 25.7 kutoka kilometa 758.6 kufikia kilometa 783.7 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025 sawa na ongezeko la asilimia 3.387.

TANROADS Mkoa wa Kagera unaendelea na utekelezaji wa miradi sita ya ujenzi wa barabara na madaraja ikiwa ni wastani wa utekelezaji wa miradi hiyo ni kati ya asilimia 2.4 na asilimia 99.

Uboreshaji wa upanuzi wa Bandari ya Bukoba

Serikali ya Awamu ya Sita inayoogozwa na Rais Dk. Samia, imetenga fedha sh. bilioni 19,544,490,352.07 kuboresha na kupanua miundombinu ya Bandari ya Bukoba ambapo utekelezaji ulianza Januari 20 mwaka 2023 na utarajiwa kukamilika Aprili 30, Mwaka huu.

Upanuzi huo na maboresho hayo, yanachochea mafanikio katika sekta ya usafirishaji kwa njia ya meli, Mathalani magati ya kupakia na kushusha mizigo na abiria yameogezeka kutoka tatu hadi tano kuanzia Novemba, 2020 had Aprili, 2025. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa jengo jipya la abiria kutaongeza uwezo wa kuhudumia abiria kutoka abiria 420 hadi abiria 733, kutaongeza eneo la maegesho ya magari kutoka magari 50 hadi 130, kuongezeka kwa urefu wa magati kutoka mita 80 hadi mita 110.

Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji

Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama vijijini, imeongezeka kutoka asilimia 83 hadi 76 kwa kipindi Novemba, 2020 wakati upatikanaji katika Manispaa ya Bukoba, umepanda kutoka asilimia 85 hadi 93 kwa Aprili. Upatikanaji wa maji Vijijini na mjini umepanda baada ya kukamilika kwa miradi iliyotekelezwa na inayoendelea kutekelezwa na RUWASA na BUWASA.

> **Upanuzi huo na maboresho hayo, yanachochea mafanikio katika sekta ya usafirishaji kwa njia ya meli, Mathalani magati ya kupakia na kushusha mizigo na abiria yameogezeka kutoka tatu hadi tano kuanzia Novemba, 2020 had Aprili, 2025. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa jengo jipya la abiria kutaongeza uwezo wa kuhudumia abiria kutoka abiria 420 hadi abiria 733, kutaongeza eneo la maegesho ya magari kutoka magari 50 hadi 130, kuongezeka kwa urefu wa magati kutoka mita 80 hadi mita 110.**

**MIRADI INAYOENDELEA KUTEKELEZWA**

Miradi 23 ya maji yenye thamani ya sh. 59,671,849,105.64, imetekelezwa mkoani Kagera kati ya hiyo, miradi mitatu yenye thamani ya sh. 3,603,732,649.62 imekamilika kwa asilimia 100, hivyo miradi 20 yenye gharama ya sh. 56,068,116,456.02, inaendelea kutekelezwa imefikia hatua mbalimbali za utekelezaji na wastani wa utekelezaji ni asilimia 61.

**MIRADI YA MAJI MIJINI**

Miradi 18 ya maji yenye thamani ya sh. 105,001,490,212.13 inatekelezwa katika Manispaa ya Bukoba na miji midogo Mkoani Kagera, ambapo miradi nne imekamilika na miradi 14 ipo hatua mbalimbali za utekelezaji kati asilimia 50 na asilimia 95.

**HALI YA USAMBAZAJI WA UMEME**

Hali ya usambazaji umeme katika Mkoa wa Kagera, imeendelea kuimarika hasa kwasababu ya kuendelea kwa utekelezaji wa miradi kabambe ya usambazaji umeme vijijini inayofadhiliwa na Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), hadi kufikia Machi mwaka huu, vijiji vyote 662 vya Mkoa wa Kagera vilikuwa vimeshafikiwa na umeme sawa na asilimia 100.

Kati ya vitongoji 3,665 vya Mkoa wa Kagera, vitongoji 1,763 vilikuwa vimeshafikiwa na huduma ya umeme hadi kufikia Machi 2025, sawa na asilimia 48, Serikali ya awamu ya sita imekamilisha ujenzi wa Kituo cha Kupoza Umeme cha Nyakanazi kilichopo wilaya ya Biharamulo ambacho kumewezesha wilaya mbili za Mkoa wa Kagera za Biharamulo na Ngara kuungwa katika Gridi ya Taifa.

Kukamilika kwa usimikaji wa mashine kubwa yenye uwezo wa 20MVA katika kituo cha Umeme cha Kyaka, kuongeza uzalishaji kutoka 20MVA kwenda 40MVA na kuwezesha Wilaya za Karagwe, Missenyi na kiwanda cha Kagera Suger kupata umeme wa uhakiki.

Serikali ya Awamu ya Sita, imeanza utekelezaji mradi wa ujenzi wa kituo cha kupoza umeme eneo la BENACO, lililopo wilaya ya Ngara na ujenzi wa laini ya kusafirisha umeme kwa msongo wa Kilovolti 220 kutoka BENACO hadi Kyaka.

Mradi huu unalenga kuziunganisha wilaya za Bukoba, Karagwe, Kyerwa, Missenyi na Muleba katika Gridi ya Taifa. Wilaya hizi kwa sasa zinapata umeme kutokea Gridi ya Uganda.

**HALI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA**

Wakala wa Umeme Vijijini (REA), ameingia mkataba wenye thamani ya sh. 398,737,500 na mtoa huduma Manjis Logistics limited wa kuuza kwa bei ya ruzuku mitungi 39,060 ya gesi ya kilo sita na vifaa vyake.

Mtungi utauzwa kwa bei ya ruzuku ya asilimia 50 ambayo ni sh. 17,500. Utekelezaji wa mkataba huo umeanza Mei, Mosi, mwaka 2025 na lengo ni kuuza mitungi 3,255 kwa kila Wilaya.

**SEKTA YA KILIMO**

Sekta ya kilimo ni chanzo kikubwa cha chakula na kipato kwa wananchi zaidi ya asilimia 80 ya Mkoa wa Kagera kwa mabadiliko ya tabia nchi Serikali ya Awamu ya Sita, imeendelea kuhakikisha wakulima wa Mkoa wa Kagera, wanabadili mtizamo na kuanza kutumia pembejeo bora za kilimo kuongeza tija katika kilimo.

**MBOLEA YA ZURUKU**

Mkoa wa Kagera hadi kufikia Aprili, mwaka huu, umetoa tani 1,482.4 za mbolea ya ruzuku iliyowanufaisha wakulima 4,839 awali Mkoa wa



# Kagera inavyojivunia mageuzi ya maendeleo

Kagera haukuwa unapata mbolea ya ruzuku.

Viuatilifu vilivyotolewa kwa lita

Mkoa wa Kagera hadi kufikia Aprili, mwaka huu, umegawa lita 732.8 za viuatilifu kwa wakulima kutoka lita 21.5 zilizogawiwa Novemba, 2020.

Zana za kilimo

Hadi kufikia Aprili, mwaka huu, maafisa ugani wenye pikipiki wameongezeka hadi 342 ikilinganishwa na maafisa 30 waliokuwa na pikipiki kwa kipindi cha Novemba, 2020.

Kwa kipindi cha Novemba, 2020 hadi aprili, 2025 magari mawili yamenunuliwa kwa Halmashauri za Muleba na Bukoba kwa idara ya kilimo.

Jumla ya vipimia udongo tano, vimenunuliwa na vinatumika kusaidia wakulima katika Wilaya ya Muleba, Bukoba, Kyerwa, Karagwe na Ngara kufikia Aprili, mwaka huu, kwani Mkoa haukuwa na vipimia udongo hapo awali.

Upatikanaji wa zana hizi umewezesha kuwafikia wakulima katika kaya 324,085 sawa na asilimia 72 ya kaya zote za Mkoa wa Kagera.

### SKIMU ZA UMWAGILIAJI

Mkoa wa Kagera una zaidi ya hekta 90,656.80 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji wa mazao ya chakula na biashara. Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia, imeendelea kuwekeza katika miundombinu ya umwangiliaji hadi kufikia Aprili, 2025, eneo linalolimwa kwa kilimo cha umwagiliaji limeongezeka na kufikia hekta 21,300 ikilinganishwa na ukubwa wa eneo la hekta 20,300 zilizokuwa zinalimwa kwa kilimo cha umwagiliaji Mkoani Kagera Novemba, 2020.

Serikali ya Awamu ya sita imewezesha kufanya upembuzi ya kinifu na usanifu kwa skimu nyingine 14 zenye hekta 19,600 katika Wilaya za Muleba, Missenyi, Biharamulo, Bukoba, Karagwe, Kyerwa na Ngara.

Uwekezaji huu, katika sekta ya kilimo umewezesha kuongeza uzalishaji wa mazao makuu ya chakula kutoka tani 3,839,775 msimu wa 2020/21 hadi kufikia tani 4,222,692 msimu wa 2024/25, uzalishaji huu uwevuka mahitaji ya chakula kimkoa wa tani 892,707, uzalishaji wa mazao ya biashara umeongezeka kutoka tani 68,928.7 msimu wa mwaka 2020/21 hadi kufikia tani 88,935 msimu wa mwaka 2024/25.

### SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

Sekta ya uvuvi na mifugo, ina mchango mkubwa wa moja kwa moja wa lishe, kipato na mchango katika uchumi wa Mkoa na wakazi wa Mkoa wa Kagera hasa ikizingatiwa kuwa asilimia 27 ya eneo la Mkoa limezungukwa na maji hususan ziwa Viktoria.

### UVUVI

Licha ya mabadiliko ya tabia nchi yanayoendelea kushuhudiwa duniani, hali ya uvuvi Mkoani Kagera ni ya kuridhisha ambapo mavuno ya samaki yameongezeka kutoka tani 26,178 Novemba, 2020 hadi kufikia tani 32,349 Aprili, mwaka huu, zenye thamani ya sh. bilioni 380.5.

Mauzo ya samaki na dagaa nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 2,873.8 hadi kufikia tani 7,555.3, ongezeko hili limechangiwa na serikali kuanzisha soko la samaki la kimataifa Wilayani Muleba, eneo la Magarini ambapo wafanyabiashara kutoka DRC. Congo, Burundi, Rwanda, Zambia na Sudani Kusini hufika na kununua samaki na dagaa.

Ufugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa

Katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, serikali ya Awamu ya Sita imejielekeza kuwezesha wananchi wa Kagera kufuga samaki kwa njia ya mabwawa na vizimba. Idadi ya mabwawa ya samaki yameongezeka kutoka mabwawa 694 hadi 724 kuanzia Novemba, 2020 kufikia mabwawa 724 Aprili, mwaka huu.

Idadi ya vizimba vya kufugia samaki vimeongezeka kutoka vizimba viwili hadi 52 kuanzia Novemba, 2020 kufikia Aprili, mwaka huu maeneo 12 yaliyotegwa kufugia samaki kwa njia ya vizimba.

Uwezeshaji wa jamii ya wavuvi

Kwa kipindi cha Novemba, 2020 hadi Aprili, mwaka huu vikundi 49 vimeundwa. Kati ya hivyo, vikundi 14 na watu binafsi nane walipewa mikopo yenye thamani ya sh. bilioni 1.713 kupitia Benki ya maendeleo ya kilimo (TADB) ya miradi ya ufugaji wa samaki kwa vizimba 52 na ununuzi wa boti tano za Uvuvi.

Ufugaji kwa njia ya Ranchi

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia imedhamiria kutumia fursa ya uwepo wa ranchi Mkoa Kagera kuwanufaisha wananchi hasa wafugaji. Serikali imewapatia wananchi hekta 2,000 ya kufuga ng'ombe kibiashara na hekta 18,709.8 ya shuguli nyingine kupisha wawekezaji baada ya kumaliza migogoro ya muda mrefu kati ya wananchi na wawekezaji.

Uwezeshaji wa vijana na mitaji ya ufugaji kibiashara

Kupitia programu ya BBT – LIFE, inayotekelezwa Mkoani Kagera katika chuo cha Mifugo LITA Karagwe, Jumla ya vijana 60 wamewezeshwa mitaji ya ng'ombe 600, elimu ya unenepeshaji na mbinu za utafutaji wa masoko ya mifugo iliyonenepeshwa.

**Ufugaji wa samaki katika vizimba na mabwawa Katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, serikali ya Awamu ya Sita imejielekeza kuwezesha wananchi wa Kagera kufuga samaki kwa njia ya mabwawa na vizimba. Idadi ya mabwawa ya samaki yameongezeka kutoka mabwawa 694 hadi 724 kuanzia Novemba, 2020 kufikia mabwawa 724 Aprili, mwaka huu.**

Baada ya kuhitimu mafunzo hayo, kila kijana amepatiwa eneo lenye ukubwa wa hekta moja katika ranchi ya Kagoma kufanya ufugaji wa kibiashara na hivyo kujikwamua kiuchumi.

### VIWANDA

Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia, imeendelea kuboresha mazingira ya kuendeleza na kuanzisha viwanda vipya Mkoani Kagera. Idadi ya viwanda vikubwa imeongezeka kutoka 11 kufikia 21 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili,mwaka huu. Idadi ya viwanda vya kati nayo imeongezeka kutoka 101 kufikia 360, kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, mwaka huu.

Viwanda vidogo vimeendelea kutoa fursa ya kujiajiri kwa wajasiriamali wapatao 3,569 Mkoani Kagera. Idadi ya viwanda vidogo vidogo imeongezeka kutoka 773 Novemba, 2020 hadi 1,370 Aprili, 2025.

### BIASHARA

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia, imeendelea kuweka mazingira bora ya ufanyaji, uendeshaji biashara na kuwezesha biashara ndogo kurasimishwa. Biashara rasmi zimeongezeka kutoka 16,376 kufikia 25,378 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, mwaka huu. Wafanya biashara wadogo (wamachinga) wanaendelea kutambuliwa na kuwekewa mazingira mazuri ya kufanya biashara zao Mkoani Kagera ikiwa ni ujenzi wa ofisi ya wanachinga katika Manispaa ya Bukoba. Idadi ya wamachinga waliotambuliwa kupitia mfumo maalum imeogezeka kutoa 1,950 hadi 2,821 kuanzia 2023 hadi Aprili, 2025.

### Uwekezaji

Serikali ya Awamu ya Sita, imejithatiti kutekeleza kwa vitengo sera ya mageuzi ya viwanda nchini Tanzania na katika Mkoa wa Kagera.

Kutokana na mazingira mazuri idadi ya wawekezaji imeongezeka kuanzia 175 hadi 275 kwa kipindi cha Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025. Miradi ya uwekezaji yenye thamani ya sh. billioni 267.16 imesajiliwa na Kituo cha uwekezaji kwa Mkoa wa Kagera inayotoa ajira 11,072.

Mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vinana na wenye ulemavu

Serikali imeendelea kuwezesha vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu Mkoani Kagera kwa kuwapatia mikopo isiyokuwa na riba inayotokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa kila Halmashauri.

Vikundi vya wanawake vinavyopata mikopo vimeongezeka kutoka 630 kufikia 1,370 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025, Vikundi vya vijana vinavyopata mikopo vimeongezeka vilikuwa 395 vimefikia 957 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, mwaka huu. Aidha, idadi ya vikundi vya watu wenye walemavu vilivyopatiwa mikopo vimeongezeka kutoka 103 hadi 150 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025.

Mikopo iliyotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu imeongezeka kutoka sh. bilioni 3.23 hadi bilioni 9.41 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili mwaka huu. Mafanikio haya yamewezesha wajasiriamali wanawake, vijana na wenye ulemavu kuboresha maisha yao na kupunguza umaskini kupitia biashara zao.

### TASAF

Serikali imeendelea kuwezesha makundi mbalimbali kiuchumi na kuondoa umaskini, Fedha zilizopokewa kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini zimeongezeka kutoka sh. bilioni 16.819 hadi bilioni 34.858 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, mwaka huu.

Kupitia mpango huu wanufaika wameongezeka kutoka 36,045 hadi 380, 035 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025, mpango huu umewezesha wanufaika kuanzisha miradi ya kujiongezea kipato kama vile ufugaji wa mbuzi, kuku, ng'ombe, biashara ndogo, kupata bima za afya za jamii, kuboresha lishe katika kaya na kuboresha makazi.

### UWEZESHAJI VIJANA

Serikali ya awamu ya sita imetoa fursa kwa vijana kwa Mkoa wa Kagera katika sekta za uzalishaji na kilimo cha kisasa cha kahawa. Vijana 300 wananufaika na Uazishwaji wa shamba la Kahawa la Vijana Makongora lenye ukubwa wa ekari 300 katika Kijiji cha Makongora kata Ruhanga ambapo jumla ya ekari 280 zimepandwa miche ya kahawa kufikia April, mwaka huu. Aidha, Kongani nne zimeanzishwa kwa ajili ya vijana katika Wilaya za Missenyi, Bukoba, Muleba na Kyerwa zilizowezesha vijana 180 kujiajiri na kuajiri wengine.

### MIRADI YA KIMKAKATI

Katika kipindi cha serikali ya awamu ya sita, imedhamiria kuufungua Mkoa wa Kagera kiuchumi kwa kutekeleza miradi ya kimkakati yenye lengo la kuboresha huduma kwa wananchi na kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri. Miradi ya kimkakati imeongezeka kutoka miradi 11 hadi 28 kuanzia Novemba, 2020 hadi Aprili, mwaka huu inayotekelezwa Mkoani Kagera.

Miradi ya kimkakati 28 ikiwemo ya ujenzi wa stendi za kisasa, masoko, kumbi za kisasa na maengesho ya magari makubwa ya mizingo yenye thamani ya sh. 6,057,218,872 inaendelea kutekelezwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.



# TRA Mkoa wa Kagera yavuka lengo ukusanyaji kodi miaka minne ya Rais Dk. Samia madarakani

**>>Yapongeza jitihada zinazofanywa na Rais Dk. Samia kuboresha ukusanyaji kodi ambao umekuwa chachu kubwa**



**Na SUPERIUS ERNEST**

MIAKA minne ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan madarakani imekuwa ya mafanikio makubwa, katika taasisi mbalimbali za Mkoa wa Kagera kwa kufanikisha malengo kusudiwa ya serikali na kuvuka lengo.

Moja ya Taasisi ambayo imefanya vizuri katika kipindi hicho ni Mamlaka ya Ukusanyaji Kodi (TRA) kanda ya Kagera ambayo imefanikiwa kuvuka lengo katika miaka minne ya uongozi wa Rais Dk. Samia.

Akielezea mafanikio hayo, Meneja wa TRA, Mkoa wa Kagera, Castrol John, alisema wanajivunia uongozi wa Rais Dk. Samia kwani ndani ya kipindi hicho wamepata mafanikio makubwa yua ukusanyaji kodi na kuvuka lengo walilokusudia.

**MAKUSANYO YA KODI KUANZIA 2020 HADI 2025**

Meneja John alisema kwa mwaka 2020 hadi 2021, walikusanya sh. milioni 73,316.42 sawa na asilimia 103.18 kati ya malengo ya kukusanya sh. milioni 71,055.6 waliyokuwa wamejiwekea.

Alisema kwa mwaka 2021/2022, walikusanya sh. milioni 94,831.11 sawa na asilimia 115.67, kati ya malengo ya kukusanya sh. milioni 81,981.94 yaliyokusudia kwa mwaka huo.

"Kwa mwaka 2022/2023 walikusanya sh. milioni 113,134.94 sawa na asilimia 90.27 kati ya malengo ya kukusanya sh. milioni 125,326.69 yaliyokuwa yamepangwa kwa mwaka huo," alisema.

Aliongeza, kwa mwaka 2023/24, walikusanya sh. milioni 119,007sawa na asilimia 101 kati ya malengo ya kukusanya sh. milioni 118,128 yaliyopangwa kufikiwa kwa mwaka huo.

Meneja John alisema, kwa mwaka 2024/25 kipindi cha Julai hadi Desemba, walikusanya sh. milioni 92,300, sawa na asilimia 114 kati ya malengo ya kukusanya sh. milioni 80,986 iliyokuwa imekusudiwa.

**MIKAKATI ILIYOTUPELEKEA KUVUKA MALENGO MWAKA 2023/2024**

Akielezea mikakati ya kufikia mafanikio hayo, Meneja John alisema, usimamizi wa matumizi ya mashine za EFD uliwasaidia kufanikisha lengo.

"Tuliendelea na ufuatiliaji wa matumizi ya EFD kwa kutumia mifumo mbalimbali kushirikiana na taasisi mbalimbali kupata taarifa.

"Kutanua wigo wa walipakodi, tuliendelea na mkakati wa kuwabaini na kuwasajili wafanyabiasahara ambao wana sifa za kusajiliwa katika wigo wa kodi," alisema.

Alitaja mikakati mingine ni ukaguzi wa ritani za kodi, ambapo Mkoa wa Kagera, uliendelea na ukaguzi ritani za VAT, kwa lengo la kuwabaini wanaotumia risiti za kughushi na kuchukua hatua.

Alisema utoaji wa elimu kila wiki, ambapo waliendelea na mipango ya kutoa elimu kila wiki kwa makundi kuchochea ulipaji kodi wa hiari kwa wafanyabiashara.

**Tuliendelea na ufuatiliaji wa matumizi ya EFD kwa kutumia mifumo mbalimbali kushirikiana na taasisi mbalimbali kupata taarifa. "Kutanua wigo wa walipakodi, tuliendelea na mkakati wa kuwabaini na kuwasajil...**

Vilevile, alisema usimamizi wa vitalu vya kodi(block management system), kuendelea na mikakati ya kuwatembelea walipakodi kupitia vitalu vya kodi (Block Management system) hii iliwasaidia kusogeza huduma karibu na walipakodi na kuongeza hari ya kulipa kodi kwa hiari.

Meneja John alitaja mkakati mwingine ni kusimamia maadili ya watumishi, waliendelea kuhimiza uzingatiaji wa maadili ya msingi ya watumishi wa mamlaka na ilisaidia watumishi kujiepusha na vitendo vyote vya uvunjifu wa maadili.

Pia, alisema kusimamia na kukusanya madeni, uliongeza kodi kuwezesha wateja wenye madeni sugu ya muda mrefu kwa kuongeza usimamizi wa karibu ulipaji wa hiari uliongezeka.

Alitaja mkakati mwingine ni kuongeza wigo wa usajili wa wafanyabiashara katika matumizi ya mashine za EFD, ilisaidia kuwabaini na kuwasajili wafanyabiashara wote wanaostahili.

Aliongeza kuwa, mkakati mwingine ni kununua na kutumia mashine za EFD na kuimarisha wigo wa kukusanya kodi.

"Kusimamia matumizi ya mifumo ya kodi,tuliendelea kuhimiza matumizi ya mifumo ya kodi hii ilisaidia kupunguza malalamiko ya wateja na kupunguza vitendo vya kimaadili katika usimamizi wa makusanyo ya kodi,"alisema.

**CHANGAMOTO**

**Utoaji hafifu wa EFD risiti**

Alieleza kuwa, kumekuwa na wafanyabiashara wasiotakakutekeleza wajibu wao wa kisheria wa kutoa risiti kila mauzo wanayofanya.

Pia, ukwepaji wa kodi kupitia mwavuli wa machinga, kumekuwa na wimbi kubwa la wafanyabiashara wakubwa kujificha katika mwavuli wa machinga hivyo kusababisha upotevu wa kodi ya serikali.

"Utumiaji wa risisti za kughushi za EFD,uwepo wa wafanyabiashara kununua risiti hizo ilikupungua kiasi cha kodi anachotakiwa kulipa hasa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) ufungaji horera wa biashara," alisema.

Alitaja jambo lingine ni kuwepo tabia ya kufunga biashara bila kufuata utaratibu pale inapotokea mlipakodi kapelekewa hati ya madai ya kodi.

Meneja John alimshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Kagera Mh Hajjat Fatma Mwassa pamoja na wasaidizi wake wote bila kuwasahau Walipakodi wote pamoja na Jumuia za wafanyabiashara TCCIA, JWT, TWCC, SHIUMA, TABOA, Vyombo vya habari na wadau wengine kwa kuhakikisha walipakodi wanalipa kodi zao kwa wakati na kwa hiari na kupelekea ongezeko kubwa la makusanyo ya kodi.







## ENZI HIZO



NDUGU Nelson Mandela, akiweka shada la maua kwenye kaburi la Rais wa Kwanza wa Zanzibar, hayati Abeid Amani Karume, katika viwanja vya Ofisi Kuu ya CCM Kisiwandui mjini Zanzibar, jana. Hiyo ilikuwa Machi 8, 1990.

UHURU ya Kijani

MAONI YA MHARIRI

# Kongole Rais Dk.Samia kwa jitihada zako za kuendeleza Mkoa wa Kagera

**Na SUPERIUS ERNEST**

KAGERA ni miongoni mwa mikoa ya kimkakati ambayo ina rasilimali nyingi za kiuchumi ambazo ni chanzo cha ukuaji uchumi wa wananchi na Taifa.

Baadhi ya rasilimali zilizopo Kagera ni ziwa victoria ambalo ni miongoni mwa chanzo kikubwa cha ukuaji uchumi.

Rasilimali zingine ni mito mikubwaa iliyosheheni maporomoko ya maji ambayo ni miongoni mwa chanzo cha kiuchumi.

Vyanzo vingine vya kiuchumi ni mazao ya biashara na chakula ikijumuisha ndizi, kahawa, mihogo, mahindi, maharage na mengineyo.

Pia, Mkoa wa Kagera ni wa kibiashara kwa sababu ya kuwa na bandari, kupakana na mataifa mengine yakiwemo Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi hivyo kuwa na muingiliano mkubwa wa kibiashara.

Pia, Kagera ina uwanja wa ndege na imeunganishwa kwa lami na mikoa mingine na mataifa hayo jirani hali inayosaidia kuchochea ukuaji uchumi.

Kwa hali hiyo inawezesha mkoa huo, kuwa wa kimkakati katika kufungua biashara kati ya Tanzania na mataifa hayo mengine, kuimarika kwa ulinzi na usalama kupitia mpaka wake na nchi jirani.

Kwa umuhimu huo, Rais Dk.Samia hajauacha Mkoa huo, ameendelea kuufungua kiuchumi kwa kuimarisha miundombinu ya usafirishaji nchi kavu, majini na angani.

Kupitia nchi kavu , Rais Dk.Samia ametoa fedha nyingi za uendelezaji wa mkoa huo, kuhakikisha barabara zinajengwa kwa kiwango cha lami kupitika vyema na kwa wepesi jambo linalolenga kuchochea ukuaji uchumi wa Taifa na wananchi.

Kuhusu usafiri na usafirishaji majini, Rais Dk. Samia ametoa fedha za kujengwa kwa meli kubwa za abiria na mizigo kutoka mwanza hadi Bukoba na zile nyingine zinazofanya kazi ziwani humo bila kusahau vivuko mbalimbali.

Kuhusu usafiri wa anga, serikali ya Rais Dk.Samia imeendelea na mkakati wa kuimarisha uwanja wa ndege wa Bukoba, kwa kuhakikisha unakuwa wa kisasa kwa kuwa na eneo la kutosha kuepusha changamoto ya kiusalama kwa wasafiri.

Mikakati mingine inayofanywa na serikali, katika kuendelea Mkoa wa Kagera na kuimarisha uwekezaji wa ndani kuanza na wanakagera wenyewe na kuvutia wengine kutoka nje.

Hilo limeshuhudiwa kupitia ofisi ya Mkuu wa Mkoa, ameanzisha tamasha la ijuka omuka, 'kumbuka nyumbani, ambalo uwakusanya wana Kagera wote na kuwaleta pamoja katika kufanya tathimini ya uwekezaji na kufahamu fursa za Mkoa huo katika kuchochea maendeleo.

Hakika tamasha hilo la kila mwaka limekuwa chachu kubwa ya kuwepo mwamko wa uwekezaji ndani ya mkoa jambo litakalo toa tija ya ukuaji uchumi kwa wananchi, Mkoa na Taifa kwa ujumla.

Katika hilo pongezi kwa serikali kupitia mkuu wa Mkoa ambaye anamwakilisha vyema Rais Dk.Samia katika kuwaunganisha wananchi wa Kagera na kufungua fursa za kiuchumi.

Ni imani yangu kuwa, jitihada hizo zikiendelea kufanyika zitainua mkoa huo kiuchumi na kuondoka katika orodha ya mikoa ya mwisho kiuchumi kuwa miongoni mwa ile jnayofanya vizuri katika kuchochea maendeleo ya wananchi.

Kongole nyingi kwa serikali ya Rais Dk.Samia kwa mageuzi hayo ya kimkakati kwa Mkoa wa Kagera naamini utekelezaji wa mikakati ikiendelea hivyo mafanikio makubwa yatafikiwa.

Rai yangu kwa wananchi na viongozi wa Mkoa wa huo ni kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali za kuinua uchumi wa wananchi, Mkoa na kuchangia pato la Taifa kupitia Mkoa huo.

Pia, pongezi kwa serikali kwa kuendelea kuimarisha ulinzi na usalama wa Mkoa huo licha ya kupakana na mataifa mengi lakini amani na usalama vimeendelea kuimarika wakati wote.

S.L.P. 9221, Dar es Salaam.
Makao Makuu: Mtaa wa Lumumba mkabala na Shule ya Msingi Mnazi Mmoja.
Chumba cha Habari:
+255-22-2183782 /FAX: 2183780
email: uhurunews@yahoo.com
uhuruadvert@gmail.com
uhurumakala@gmail.com

Kaimu Mhariri Mtendaji: ____ 0784 - 333186
Naibu Mhariri Mtendaji: ____ 0784 - 599717
Mhariri wa Habari: ____ 0657- 913894
Mhariri Msanifu : ____ 0784 - 599717
Mhariri wa Michezo: ____ 0718 - 611700

IDARA YA BIASHARA
Meneja Biashara: ____ 0683 - 378522
Meneja Matangazo: ____ 0765 - 142207
Kaimu Meneja Mauzo na Usambazaji: ____ 0715 - 313263

REDIO UHURU FM (PMCL)
uhurufmnews@gmail.com
Kaimu Mkurugenzi Uhuru FM: ____ 0765 – 383757
Kaimu Mhariri Mkuu Uhuru FM: ____ 0713 - 248640

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

STAMIGOLD Company Limited



**Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# MGODI WA DHAHABU WA STAMIGOLD



**Meneja Mkuu wa Mgodi Bw. Ali Said Ali**



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
STAMIGOLD Company Limited

# MGODI WA DHAHABU WA STAMIGOLD



Meneja Mkuu wa Mgodi
Bw. Ali Said Ali



## UMILIKI

STAMIGOLD COMPANY LIMITED (STAMIGOLD) ni Kampuni tanzu ya Shirika la Madini la Taifa (STAMICO).

STAMIGOLD ilianzishwa tarehe 28 Oktoba, 2013 na inamilikiwa kwa ubia kati ya STAMICO na Msajili wa Hazina.

Kampuni hii inajukumu la kuendeleza mgodi wa dhahabu wa STAMIGOLD Biharamulo Mine (SBM) ambao ulirithiwa kutoka kampuni ya Pangea Minerals LTD iliyokuwa mmiliki wa awali kupitia Leseni Maalum ya Uchimbaji Na. SML157/2003.

Ni mgodi unaoendeshwa na wazawa kwa mafanikio inayojenga sababu kwa wataalamu wetu kuaminika katika usimamizi wa migodi.

## MADINI

**Tafiti zinazoendelea zinatoa matumaini ya kurefuka kwa maisha ya mgodi kwa kugundua maeneo mapya ya uchimbaji. Mgodi unatenga fedha kwa ajili ya kuwezesha tafiti za kina.**

## SHUGHULI ZA MGODI

Ili kuendeleza mgodi huu, wataalamu wanabuni mbinu za kuongeza uzalishaji kwa lengo la kurefusha maisha ya mgodi. Kwa msingi huo, shughuli za utafiti wa miamba yenye madini ya dhahabu zimepewa kipaumbele, ambapo wataalamu wa ndani wanashirikiana na taasisi za Geological Survey of Tanzania (GST) na STAMICO ili kufanikisha kazi hii.

Tafiti zinazoendelea zinatoa matumaini ya kurefuka kwa maisha ya mgodi kwa kugundua maeneo mapya ya uchimbaji. Mgodi unatenga fedha kwa ajili ya kuwezesha tafiti za kina.

Uzalishaji wa madini ya dhahabu katika mgodi wa STAMIGOLD, Wilayani Biharamulo unaimarika mwaka hadi mwaka.

## MAFANIKIO

Tangu kuanzishwa kwa STAMIGOLD imeweza kufanikiwa katika mambo mbalimbali kama;

Ajira kwa Wazawa



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
STAMIGOLD Company Limited



# MGODI WA DHAHABU WA STAMIGOLD

**WAZAWA**

**Wakandarasi wazawa wamepewa fursa ya kufanya biashara na mgodi. Wametoa ajira kupitia kampuni zao. Kwa kufanya hivyo wameshirikiana na Serikali, ambayo mipango yake ni kuongeza fursa za ajira hasa kwa vijana.**

STAMIGOLD ni Mgodi pekee wa Serikali ambao una zaidi ya waajiriwa 600 na wote ni raia wa Tanzania, Hayo ni mafanikio katika nchi yetu kwa ujumla na ni sehemu ya kujivunia.

Wakandarasi wazawa wamepewa fursa ya kufanya biashara na mgodi. Wametoa ajira kupitia kampuni zao. Kwa kufanya hivyo wameshirikiana na Serikali, ambayo mipango yake ni kuongeza fursa za ajira hasa kwa vijana.

Wazabuni wa ndani ya nchi wanao shirikiana na Mgodi wanaendelea kunufaika na Mgodi kwa kuendelea kuzalisha ajira nyingi kwa watanzania

Mmoja wa wataalamu katika mgodi huo Fred Makwebeta "amesema mgodi huu kuwa mikononi mwa Serikali imechangia fursa nyingi kwa wananchi pia mgodi wa STAMIGOLD una miradi mingi iliyopo na inayoendelea kama sehemu ya faida wanayoipata".

**KUPUNGUZA GHARAMA ZA UZALISHAJI**

Kabla ya mgodi kuunganishwa kwenye umeme wa gridi ya taifa, mgodi wa STAMIGOLD ulitumia gharama kubwa kwenye nishati ya umeme kwa ajili ya uendeshaji wa mgodi hasa mitambo.

Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini walishiriki katika kuhimiza upatikanaji wa mradi wa umeme STAMIGOLD kwa kutambua umuhimu wa mradi huu.

Sasa mgodi huo unatumia umeme kutoka Shirika la Umeme Tanzania Tanesco tofauti na zamani, ambapo nishati hiyo ilizalishwa kwa gharama kubwa ya mafuta.

Baada ya mgodi kuunganishwa na umeme kwa gharama za Serikali, wataalamu wanasema matumizi ya mwezi katika uendeshaji wa mitambo ya kuzalisha dhahabu yameshuka kwa kiwango

**Baada ya mgodi kuunganishwa na umeme kwa gharama za Serikali, wataalamu wanasema matumizi ya mwezi katika uendeshaji wa mitambo ya kuzalisha dhahabu yameshuka kwa kiwango kikubwa.**









# MGODI WA DHAHABU WA STAMIGOLD


Zahanati ya Nampalahala


Vyoo vya Zahanati ya Nampalahala

## FURSA

**Kwa upande wa pili mgodi wa STAMIGOLD umeingia kwenye orodha ya walipaji wakubwa wa umeme katika mkoa wa Kagera kwenye Shirika la Umeme (Tanesco) na katika hatua hii wana jambo la kushauri hasa kwa watumiaji wakubwa wa aina yao waliowekeza kwenye maeneo magumu kufikika.**

kikubwa.

Kupitia mipango yao ya kupunguza gharama za uendeshaji, wataalamu wanasema baada ya kupata chanzo kipya cha umeme wamefanikiwa kuokoa mamilioni ya shilingi kwa asilimia zaidi ya sitini kwa mwezi.

Kwa upande wa pili mgodi wa STAMIGOLD umeingia kwenye orodha ya walipaji wakubwa wa umeme katika mkoa wa Kagera kwenye Shirika la Umeme (Tanesco) na katika hatua hii wana jambo la kushauri hasa kwa watumiaji wakubwa wa aina yao waliowekeza kwenye maeneo magumu kufikika.

STAMIGOLD kama mmoja wa wekezaji wafikiriwe kupata unafuu kwenye gharama za malipo ya umeme

Wanasema kama ilivyo kwa miradi ya umeme Vijijini kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA) pia nao wanatakiwa kupata punguzo ya gharama za umeme kwa kuwa uwekezaji wao uko Vijijini.

Wanasema bila mkono wa Serikali kuhakikisha mgodi huo unaunganishwa na umeme wa Tanesco, ingeweza kuathiri zaidi ufanisi wa mgodi huo ambao kwa kiwango kikubwa unategemea nishati ya umeme.

### JAMII INANUFAIKAJE

Wananchi wa Wilaya ya Biharamulo, Mkoani Kagera Wanajivunia uwekezaji wa Serikali katika mgodi wa STAMIGOLD. Baadhi ya miradi ya Jamii imetekelezwa huku fursa mbalimbali kufunguka.

### KUBORESHA MIUNDOMBINU

Miundombinu ya barabara imeimarishwa kwa kupitia Mgodi wa STAMIGOLD katika vijiji vinavyozunguka Mgodi. Hivyo wananchi wamepunguziwa adha ya kusafiri kwa muda mrefu.

### AFYA

Kwa kupitia Mgodi wa STAMIGOLD, Ujenzi wa Zahanati katika kijiji cha Nampalahala Wilaya ya Bukombe umesaidia sana wananchi, Kwani wanapata huduma zote za kiafya bila kupata changamoto ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya

Kwa njia hiyo mgodi wa STAMIGOLD umechangia mafanikio ya Serikali ya awamu


Kuchangia kukuza uchumi kwa jamii inayotuzunguka, pamoja na misaada mbali mbali kwa elimu, afya na miundo mbinu






Shule ya Sekondari Mavota - Kaniha



Vyoo vya Shule ya Sekondari Mavota - Kaniha

# MGODI WA DHAHABU WA STAMIGOLD

ya sita ya kuongeza kasi yake ya kupunguza vifo vya wanawake wajawazito na watoto Kwa kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi.

### JUHUDI ZA STAMIGOLD KUKUZA ELIMU KWA JAMII

Shule ya Sekondari Mavota ni miongoni mwa Shule nzuri na ya kisasa iliyojengwa na Mgodi wa STAMIGOLD, ikiwa ni kurudisha fadhila katika jamii kwenye nyanja ya elimu.

Utekelezaji wa ujenzi huu ni mafanikio ya kuingia makubaliano na Halmashauri ya Biharamulo kupitia mpango wa Uwajibikaji kwa mmiliki wa Leseni (CSR). Kwa kutambua mchango wa elimu katika jamii zetu. Mgodi umejenga shule karibu na vijiji ili kupunguza changamoto wanazopata watoto kutembea umbali mrefu.

### MAFUNZO KWA VITENDO

Sambamba na hilo mgodi wa dhahabu wa STAMIGOLD inapokea wanafunzi kwa mwaka zaidi ya 100 kwa ajili ya kujifunza kwa vitendo (Field na Internship). Hii inasaidia kuandaa wataalamu katika sekta ya madini kwa manufaa ya taifa baadae.

Aidha, mgodi hushiriki katika utoaji wa elimu kwa jamii katika sekta mbalimbali kama afya, uchumi, na kilimo katika vijiji vinavyozunguka mgodi. Wataalamu mbalimbali hutumia majukwaa haya pia kuwaelimisha wananchi kuhusu manufaa yanayotokana na uwepo wa mgodi katika maeneo yao.

Mmoja wa wataalamu na viongozi katika mgodi huu Mhandisi Godfrey Lweyemamu, anasema "huu ni mgodi shule ambao wataalamu wa Kitanzania wanafundishwa kwa vitendo, na wamekidhi mahitaji ya soko la ndani na nje. Hii inathibitisha kuwa tunaweza".

Pia anasema ni uwekezaji mzuri uliofanywa na Serikali. Unafuta dhana ya kwamba nchi haina wataalamu wenye weledi wa kutosha kusimamia na kuendesha migodi ya kuchimba madini. Anabainisha kwamba mgodi wa STAMIGOLD ni kipimo cha



Wanafunzi kutoka vyuo mbalimbali wakijifunza katika mgodi wa Stamigold

**WATAALAMU**

**Mmoja wa wataalamu na viongozi katika mgodi huu Mhandisi Godfrey Lweyemamu, anasema "huu ni mgodi shule ambao wataalamu wa Kitanzania wanafundishwa kwa vitendo, na wamekidhi mahitaji ya soko la ndani na nje. Hii inathibitisha kuwa tunaweza**

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

STAMIGOLD Company Limited

# MGODI WA DHAHABU WA STAMIGOLD





uwezo wa wataalamu wazawa.

**FURSA ZA BIASHARA KWA WANANCHI**

Uendeshaji wa mgodi wa STAMIGOLD unatanguliza maslahi kwa wananchi ambao ndio wanamiliki kitega uchumi hicho, kupitia Serikali yao inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Baada ya Serikali kuanzisha mgodi huu walikubaliana kupunguza gharama za uendeshaji kwa kutoa manunuzi yasiyo ya lazima kutoka nje badala yake kufanya manunuzi ya ndani.

Badala yake mahitaji hayo na mengine yanatoka hapa nchini. Wananchi wamepewa fursa ya kufanya biashara na mgodi wa STAMIGOLD kwa taratibu rafiki ambazo ziko ndani ya uwezo wao.

Fursa kwa wananchi kufanya biashara na mgodi, imechochea Kilimo cha mbogamboga na matunda na wengine wamepewa mafunzo ya jinsi ya kuongeza thamani ya mazao yao. STAMIGOLD imefanikiwa pia kuwawezesha wachimbaji wadogo waliopo karibu na mgodi kwa kuwapa elimu na kuwasaidia kufanya tafiti za kitaalamu zaidi ili waweze kufikia malengo yao katika shughuli zao za uchimbaji.

Wachimbaji wadogo wamesaidiwa na wataalamu wa mgodi kupunguza gharama kwa kupeleka sampuli maabara kwa ajili ya vipimo, badala yake wanaleta mgodini bila malipo na kupata ushauri wa kitaalamu zaidi. Hii imesaidia kupunguza gharama na muda wa kufanya utafiti kwa muda mrefu.

**GHARAMA**

**Wachimbaji wadogo wamesaidiwa na wataalamu wa mgodi kupunguza gharama kwa kupeleka sampuli maabara kwa ajili ya vipimo, badala yake wanaleta mgodini bila malipo na kupata ushauri wa kitaalamu zaidi. Hii imesaidia kupunguza gharama na muda wa kufanya utafiti kwa muda mrefu.**

**MAONI YA WATAALAMU**

Pamoja na mipango ya wataalamu kulenga kunufaisha wananchi wengi zaidi, zipo baadhi ya changamoto zinazohitaji mjadala na hatimaye kupata ufumbuzi wa kudumu ambao utaongeza ufanisi wa kazi kwenye mgodi wa STAMIGOLD.

Wanapendekeza uwepo utaratibu rafiki wa ununuzi kwa kuwa wako kwenye soko la ushindani. Utaratibu wa sasa (NESTI) unawachelewesha kuingia sokoni. Hawawezi kushindana na migodi mingine ambayo taratibu zao za ununuzi hazichukui muda mrefu.

Wanasema sio rahisi kushindana na kampuni nyingine za uchimbaji wa madini, ambazo uamuzi wa kununua kipuli cha mtambo unafanyika kwa saa chache. Kwa ununuzi ya kipuli kile kile wao lazima waombe kupitia mfumo wa tenda. Mzabuni anaweza kupatikana miezi miwili baadaye.

Pamoja na kuchangia shughuli za maendeleo kwenye jamii zinazo zunguka eneo la mgodi wa uchimbaji wa madini ya dhahabu wa STAMIGOLD, pia unatoa michango wa shughuli za maendeleo kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
# HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA









Kamishna wa Uhifadhi - TANAPA
Musa Nassoro Kuji

# MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (2021/2022 – 2024/2025) YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
**HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA**

# MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA NDANI YA HIFADHI ZA TAIFA BURIGI-CHATO, IBANDA-KYERWA NA RUMANYIKA-KARAGWE - MKOA WA KAGERA

Makala haya, yanakusudia kuelezea mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Hifadhi za Taifa tatu (3) za Mkoa wa Kagera ambazo ni Burigi-Chato, Ibanda-Kyerwa na Rumanyika_Karagwe kama ifuatavyo:

## A.HIFADHI YA TAIFA BURIGI-CHATO

Hifadhi za Taifa Burigi – Chato ilianzishwa tarehe mwaka 2019 kwa Matangazo ya Serikali Namba (GN) 508 kwa kupandisha hadhi kwa yaliyokuwa mapori ya akiba ya Biharamulo, Burigi na Kimisi. Hifadhi ina ukubwa wa kilometa za mraba 4,707.

Inapatikana Kaskazini Magharibi mwa Tanzania katika Wilaya za Biharamulo, Muleba, Ngara na Karagwe za Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Chato ya Mkoa wa Geita. Aidha, Hifadhi ya Taifa Burigi – Chato ni ya nne (4) kwa ukubwa kati ya Hifadhi za Taifa zote 21 zinazosimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) nchini.

Malengo ya kuanzishwa kwa Hifadhi hii ni sehemu ya jitihada za Serikali za kuimarisha Uhifadhi na Ulinzi wa maliasili, kukuza utalii, kuongeza pato la Taifa na kuchochea ukuaji wa uchumi/ maendeleo ya wanachi.


## JINSI YA KUFIKA HIFADHINI

Hifadhi Ya Taifa Burigi-Chato inafikika kwa barabara; (Dodoma – Bukoba, Mwanza – Biharamulo, Uganda/Mutukura – Karagwe (lango la Ruhita), Rusumo – Nyungwe, n,k). Kwa ndege kupitia viwanja vya ndege Geita/ Chato, Bukoba, Biharamulo na Ngara. Pia, Hifadhi ina kiwanja cha ndege ndogo eneo la Nkonje ndani ya Hifadhi. Makao makuu ya Hifadhi yapo Biharamulo mjini.

## AINA ZA UTALII NDANI YA HIFADHI.

Shughuli za utalii zinazofanyika ni pamoja na: Utalii wa picha na kuangalia wanyama kwa gari nyakati za mchana na usiku (game drive), utalii wa Kitamaduni na utalii wa kutembea




Ramani Na. 1 : Mahali inapatikana Hifadhi ya Taifa Burigi - Chato

kwa miguu kuangalia vivutio (Walking safari) na Utalii wa Boat ziwa Burigi na Ziwa Victoria. Hifadhi inavyo vivutio vingi ikiwa ni pamoja Big Four katika wale Big Five (simba, chui, tembo, nyati) na makundi mbalimbali ya wanyama kama vile Pundamilia, Twiga, Swala korongo, Swala pala, tohe, pofu ngiri, fisi, wanyamapori wa kipekee mbega wekundu (ashy red colobus) n.k. Pia, Mandhari nzuri ya kuvutia yakichagizwa na milima, mabonde na nyanda za nyasi fupi na ndefu pamoja na mistu minene katika hasa kanda ya Biharamulo na Burigi.

## MAFANIKIO KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Katika kipindi cha miaka minne (4) cha serikali ya awamu ya sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hifadhi imepokea Jumla ya Tzs. 6,875,339,384.46 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na malazi ya wageni Hifadhi kama ifuatavyo:

I. Ujenzi wa Nyumba za Kulala wageni (Cottages) 6 (2 in 1) yenye uwezo wa kulaza watalii 24 kwa siku zilizogharimu jumla ya Tshs

**Katika kipindi cha miaka minne (4) cha serikali ya awamu ya sita chini ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hifadhi imepokea Jumla ya Tzs. 6,875,339,384.46 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na malazi ya wageni Hifadhi kama ifuatavyo:**





Sehemu ya Miundombinu ya Malazi (Cottages) ya Wageni Eneo la Nkonje

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
**HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA**

# MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE





**Baadhi ya mahema ya kudumu kwa ajili ya malazi ya wageni ndani ya hifadhi**

745,247,880.00

1. Ujenzi wa Mahema ya kudumu 6 ya kulaza wageni, hema moja la chakula na mahema mawili ya wahudumu yaliyogharimu Tshs 498,829,827.26.

I. Ujenzi wa jengo la kutolea taarifa za Hifadhi kwa wageni lilogharimu Tshs 392,882,227.20

II. Ujenzi wa Kambi za Askari uliogharimu Tshs 218,793,338.00 kwa ajili ya kuimalisha ulinzi wa maliasili.

III. Ujenzi wa matenki mawili ya chini ya kuvunia maji katika vituo viwili vya askari nyungwe na masheshe yaliyogharimu Tshs 19,586,112.00.

IV. Ujenzi za barabara Hifadhini (kilometa 225) ambazo ni GOFU – KATETE (KM. 30); MADARAJA 6 – RUIZA (KM. 45); NYUNGWE – NKONJE (KM. 90); RUHITA – NKONJE (KM. 25) na KIGOMBE – NZUGURUMA (SWAMP) – KM. 35. Zote zikigharimu Jumla Tzs. 5,000,000,000.00 (Bilioni 5).

V. Kuimarika kwa Uhifadhi na kuongezeka kwa jamii mbalimbali za wanyamapori Hifadhini

VI. Kuongezeka kwa watumishi (kwa zaidi ya 40%).

VII. Kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka watalii 45 (2018/2029) hadi watalii 905 (2023/2024)





**Baadhi ya Wanyamapori wanaopatikana Hifadhi ya Taifa Burigi-Chato**



**Jengo la kutolea taarifa kwa wageni eneo la Katete**



**Barabara ya Kigombe-Nzuguruma (Swamp)**

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII
## HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA

# MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (2021/2022 – 2024/2025) YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

**MKUU WA HIFADHI YA TAIFA BURIGI-CHATO**




Watalii wa ndani na wa nje wakifanya Utalii Nyakati Tofauti – Burigi-Chato

**B.HIFADHI YA TAIFA IBANDA-KYERWA**

Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kyerwa ilianzishwa tarehe 05.07.2019, kwa tangazo la Serikali namba 509. Hifadhi ina ukubwa wa kilomita za mraba 294. Hifadhi ilipandishwa hadhi kutoka kwa lililokuwa pori la akiba la Ibanda lililoanzishwa mwaka 1972. Hifadhi iko kaskazini magharibi mwa Tanzania, inazungukwa na na mto Kagera kutoka mashariki hadi magharibi mwa Hifadhi. Mto Kagera unatumika kama mpaka wa Hifadhi na nchi za Rwanda na Uganda pia sehemu ya mto Kagera inatenganisha Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kryerwa (Tanzania) na Hifadhi ya Taifa Akagera ya nchini Rwanda. Eneo lote la Hifadhi liko katika wilaya ya Kyerwa, mkoa wa Kagera. Makao makuu ya Hifadhi yapo "Murongo" umbali wa kilomita 70 kutoka makao makuu ya Wilaya Kyerwa na kilomita 210 km kutoka Bukoba mjini.

**AINA ZA UTALII NDANI YA HIFADHI.**

Shughuli za utalii zinazofanyika ndani ya hifadhi kwa mtalii anapotembelea hifadhi ni pamoja na utalii wa picha na kuangalia wanyama kwa gari nyakati za mchana na usiku( game drive), utalii wa Kitamaduni na utalii wa kutembea kwa miguu kuangalia vivutio (Walking safari).

Hifadhi inavyo vivutio vingi ikiwa ni pamoja na makundi mbalimbali ya wanyamapori kama vile Chui, Nyati, Swala korongo, Swala pala, tohe, pofu ngiri, fisi, nyani , ngedere aina zaidi ya 200 za ndege , Mandhari nzuri ya kuvutia yakichagizwa na uwanda wa nyasi fupi na ndefu Pamoja mistu michache katika uwanda wa mto Kagera.

**MAFANIKIO YA HIFADHI YA TAIFA IBANDA-KYERWA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (2021-2025)**

Katika kipindi cha Uongozi wa Mhe. Dr. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sekta ya Uhifadhi na Utalii katika Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kyerwa tumefanikiwa kupata fedha na kutekeleza miradi yenye thamani ya Jumla ya Tzs 4,432,137,696 kama ifuatavyo:

Ujenzi wa lango la watalii kuingia hifadhini (Kifurusa Complex Gate) ambalo limefikia 80% kukamilika ukijumuisha nyumba 5 za watumishi (2 kwa 1, 2,4 kwa 1, 3), visima 2 vya maji, maeneo 2 ya maegesho wakati wa kutoka na kuingia katika lango hilo, ofisi za ukaguzi wa nyaraka na malipo ofisi ya mhasibu, ofisi za askari kuingia na kutoka, ofisi ya tehama, ofisi ya afisa utalii na msaidizi wake, ujenzi wa barabara za mzunguko katika lango yenye urefu wa kilomita 2 pamoja na mfumo wa umeme vyote kwa pamoja vinagharimu thamani ya Tzs 3,500,000,000.00 (bilioni 3.5)

i. Ukarabati mkubwa wa nyumba mbili za watumishi Murongo ( Major

**Hifadhi inavyo vivutio vingi ikiwa ni pamoja na makundi mbalimbali ya wanyamapori kama vile Chui, Nyati, Swala korongo, Swala pala, tohe, pofu ngiri, fisi, nyani , ngedere aina zaidi ya 200 za ndege , Mandhari nzuri ya kuvutia yakichagizwa na uwanda wa nyasi fupi na ndefu Pamoja mistu michache katika uwanda wa mto Kagera.**



Eneo la maegesho ya magari wakati wa kutoka Hifadhini pamoja na choo katika mradi wa kifurusa complex gate



Nyumba za watumishi baada kufanyiwa ukarabati mkubwa ( major rehabilitation)



Makundi ya Nyati ni mojawapo ya vivutio vilivyopo Hifadhi ya Taifa Ibanda-Kyerwa



Ujenzi wa lango la watalii (Kifursa Complex Gate)

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
**HIFADHI ZA TAIFA TANZANIA**

# MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (2021/2022 – 2024/2025) YA MHE. DKT. SAMIA SULUHU HASSAN

Rehabilitation) tsh 351,454,720.00

ii. Matengenezo ya kilomita 45 za barabara Kutoka kifurusa hadi nchi tatu kupitia Kigaga na Rutungu -nchi tatu kupitia uwanja Kagaga zilizogharimu Tzs 580,682,976

iii. Kuimarika kwa ulinzi wa Maliasili za Hifadhi kutokana na uwepo wa vitendea kazi kazi mbalimbali ambavyo vilitolewa na serikali kama vile magari 2 mapya (1 utawala na 1 doria) pamoja na silaha hivyo basi hifadhi kuwa na magari 7 yanayofanya kazi.

iv. Serikali imetoa fedha za kutosha za kuendesha kazi mbalimbali za Hifadhi ikiwemo kazi za doria, kazi za utawala na huduma kwa watumishi.

**MKUU WA HIFADHI YA TAIFA IBANDA-KYERWA**

### C.HIFADHI YA TAIFA RUMANYIKA-KWARAGWE

Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe ilianzishwa tarehe 05.07.2019, kwa tangazo la Serikali namba 510 ikiwa na kilomita za mraba 247. Hifadhi ilipandishwa hadhi kutoka lililokuwa Pori la Akiba la Rumanyika Orugundu lililoanzishwa mwaka 1974.

Jina la Hifadhi linatokana na chifu wa kabila la Wanyambo Orugundu I aliyetawala himaya ya Karagwe kuanzia mwaka1855 hadi 1882. Eneo lote la Hifadhi liko katika wilaya ya Kyerwa, mkoa wa Kagera.

### AINA ZA UTALII NDANI YA HIFADHI

Shughuli za utalii zinazofanyika Hifadhini ni: Utalii wa kutwa wa kuangalia wanyama kwa gari, utalii wa kuendesha magari wakati wa usiku, utalii wa Kitamaduni na utalii wa kutembea kwa miguu kuangalia vivutio (Walking safari).

Hifadhi inavivutio vingi ikiwa ni pamoja na msitu wa kiikweta wenye miti mbalimbali, makundi mbalimbali ya wanyama kama vile Chui, Nyati, Nzohe, Fisi maji, Nyani, Bwea, Kicheche, Digidigi, Milima, Mabonde mazuri ya kuvutia, Mabawa yenye Samaki aina ya perege/sato, na Kambale. Ndege wa kuvutia aina mbalimbali kama; Superb starling, crowned crane, grey heron, bata maji, weavers, wag tail na Vipepeo aina mbalimbali.

### JINSI YA KUFIKA HIFADHINI

Hifadhi inafikika kwa njia mbili, usafiri wa anga na barabara;

i. Kwa njia ya anga, Hifadhi inafikika kupitia kiwanja cha ndege cha Bukoba na Chato

ii. Kwa njia ya Barabara, hifadhi inafikika kutokea Bukoba kwa kupitia Kyaka, Omurushaka hadi lango

iii. Nyakatuntu umbali wa kilometa 185. Pia kutokea Barabara ya Kayanga (Mkakorongo), Kigorogoro hadi lango la Nyakatuntu umbali wa kilometa 85. Aidha kupitia boda ya Uganda iliyopo Kikagati/Murongo hadi lango la Rugasha umbali wa kilometa 8.

### MAFANIKIO YA UHIFADHI NA UTALII KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (2021-2025)

Katika kipindi cha Uongozi wa Mh. Dr. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sekta ya Uhifadhi na Utalii katika Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe tumetekeleza miradi mbalimbali na kuimarisha shughuli za utawala na usimamizi wa Hifadhi. Zaidi ya Tzs. 451,035,174.82 zilitolewa kwa kutekeleza miradi na maboresho mbalimbali ya Hifadhi kama ifuatavyo:

i. Ujenzi wa nyumba za watumishi katika kituo cha Nyakatuntu na hivyo kuboresha huduma ya malazi kwa watumishi ulioghalimu kiasi cha shilingi za Kitanzania 231,004,114.82

ii. Uboreshaji wa miundombinu ya utalii -Barabara na njia (Trails) za kupita watalii ndani ya Hifadhi. Serikali imetoa pesa za kitanzania 220,031,060.00 Kwa ajili ya utengenezaji wa barabara ya Rugasha hadi Chababara yenye urefu wa kilomita 19.2

iii. Kuimarika kwa ulinzi wa Maliasili za Hifadhi kutokana na uwepo wa vitendea kazi kazi mbalimbali ambavyo vilitolewa na serikali kama vile magari 4 (1 utawala na 3 doria), silaha.

iv. Kuongezeka kwa watumishi kwa zaidi ya asilimia 25%.

v. Kuimarika kwa ulinzi na usalama wa nchi kutokana na Hifadhi ya Taifa Rumanyika-Karagwe kama sehemu ya ardhi ya nchi ya Tanzania kulindwa vizuri.

**MKUU WA HIFADHI YA TAIFA RUMANYIKA-KARAGWE**



**Ujenzi wa Kalavati katika mradi wa barabara ya kifurusa nchi tatu kupitia kigaga**

### B. GHARAMA ZA UTALII KWA HIFADHI ZA TAIFA BURIGI-CHATO, IBANDA-KYERWA NA RUMANYIKA-KARWAGWE

Gharama za kuingia na kufanya utalii katika Hifadhi hizi zote tatu kwa kutegemeana na umri wa mtalii ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini.

**Hifadhi inavivutio vingi ikiwa ni pamoja na msitu wa kiikweta wenye miti mbalimbali, makundi mbalimbali ya wanyama kama vile Chui, Nyati, Nzohe, Fisi maji, Nyani, Bwea, Kicheche, Digidigi, Milima, Mabonde mazuri ya kuvutia, Mabawa yenye Samaki aina ya perege/sato, na Kambale. Ndege wa kuvutia aina mbalimbali kama; Superb starling, crowned crane, grey heron, bata maji, weavers, wag tail na Vipepeo aina mbalimbali.**

### HITIMISHO

Tunaishukuru serikali ya awamu ya sita chini ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada kubwa zinazofanywa kwa kutoa fedha nyingi za kuendeleza miundombinu ya utalii, uboreshaji wa barabara na kuongeza watumishi katika Hifadhi zetu. Ni matarajio yetu kuwa Hifadhi hizi katika kipindi kifupi kijacho zitakuwa miongoni mwa Hifadhi zinazoingiza wageni wengi na kuiingizia serikali mapato makubwa hapa nchini. Aidha, Hifadhi zitakuwa zinaongeza fursa na ukuaji wa uchumi wa Kagera na Kanda ya ziwa.

Mh. Rais aliandaa filamu ya 'Tanzania The Royol Tour' na 'Amazing Tanzania' ambazo zimekuwa na mafanikio makubwa ya kutangaza vivutio vya utalii wa Tanzania na fursa za uwekezaji katika nchi yetu. Idadi ya watalii katika Hifadhi zetu zote imeongezeka sana.

Mhe. Rais amekuwa na maono makubwa katika kuendeleza sekta ya Uhifadhi wa Maliasili na kukuza Utalii nchini. Hivyo watumishi na Menejimenti za Hifadhi za Taifa Burigi-Chato; Ibanda-Kyerwa, Rumanyika-Karagwe na Shirika (TANAPA) tuna imani kubwa na Mh. Rais wetu, hivyo tunaungana na watanzania kumpongeza kwa kuteuliwa kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka mitano ijayo kwani tunaamini mambo makubwa yataenda kufanyika katika sekta hii ya Uhifadhi wa Maliasili na Utalii hasa katika Hifadhi hizi za Mkoa wa Kagera.



**Jengo la kituo cha doria Nyakatuntu lenye uwezo wa kutoa huduma ya malazi kwa askari 18.**



**Mradi wa barabara ya Rugasha-Nyakabila kwa ajili ya utalii na doria za ulinzi.**

# Makala ya Utekelezaji wa SIDO Kagera wa Miaka 4 ya Dr .Samia Suluhu Hasani




**1. IDADI YA VIWANDA VILIVYOANZISHWA KATIKA SEKTA YA KUONGEZA THAMANI MAZAO YA KILIMO YA MKOA WA KAGERA**

• Viwanda vidogo na vya kati vilivyo anzishwa : 211
• Aina za Mazao: Mazo yanayo sindikwa na Viwanda hivi ni kahawa, ndizi, asali, mahindi, mihogo,Parachichi na viazi vitamu.



**3. IDADI YA MIKOPO NA THAMANI ILIYOPEWA**

•Mikopo: Jumla ya mikopo kwa wajasiriamali iliyo tolewa ni 196
•Thamani ya Mikopo: Mikopo hii ilikuwa na thamani ya 345milioni ,mikopo hiyo ilisaidia katika kuanzisha na kuendeleza viwanda.




**2. USHAURI ULIO TOLEWA KWA KIBIASHARA NA KIUFUNDI KWA WAJASIRIAMALI 904**

•Ushauri wa Kibiashara: Ushauri wa kibiashara uliopewa wajasiriamali, ikiwa ni pamoja na Urasimishaji wa biashara kupitia BRELA ,TBS , Mkemia Mkuu wa serikali ,NEMC ,Halimashauri zote za Mkoa wa Kagera na masoko, usimamizi wa fedha, na mikakati ya biashara.
•Ushauri wa Kiufundi: ushauri wa kiufundi, kama vile Mafunzo ya teknolojia za uzalishaji,usambazaji wa teknolojia vijijini na usimikaji wa mitambo ya uzalishaji Viwandani



**4.TEKNOLOJIA ZILIZOZAMBAZWA:**

Jumla ya teknolojia 13 zilizozambazwa kwa ajili ya kusindika mazao kama kahawa, ndizi, asali, Parachichi,mahindi, mihogo, na viazi vitamu.



Mafunzo ya ujasirimali wa wanawake wasinikaji wa mazao ya dagaa na Samaki

**5.MAFUNZO KWA WAJASIRIAMALI :**

•Idadi ya Mafunzo yaliyo tolewa ni 82
•Wajasiriamali walio pewa mafunzo ni 1,968 ambayo yamechochea uanzishwa wa wa Viwanda na biashara zilizo rasmi

**6. PICHA ZA VIWANDA NA MATUKIO**







RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency





Mhe. Samia Suluhu Hassan
Rais wa Jamhuri ya
Muungano wa Tanzania



# MAFANIKIO YA RUWASA MKOA KAGERA MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA

WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

*"Maji Bombani"*

RUWASA






# MAFANIKIO YA RUWASA MKOA KAGERA MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA

**>>Wafikisha maji kwa asilimia 83 ya wakazi wote wa Kagera**

**>>Yamshukuru Rais Dk. Samia kwa kutoa mabilioni ya utekelezaji miradi**

**Na SUPERIUS ERNEST**

LENGO la Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ni kuwapatia huduma ya maji safi na salama wananchi waishio vijijini kwa asilimia 85 na asilimia 95 maeneo ya Mijini ifikapo Desemba mwaka 2025.

Malengo hayo ni kwamujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ya mwaka 2020 hadi 2025, iliyoangazia utekelezaji wa miradi ya sekta mbalimbali ikiwemo ya maji.

Katika kipindi cha miaka hiyo minne, serikali imetoa fedha kiasi cha sh. bilioni 79,839,298,567.10 ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kuongeza upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama.

Mafanikio kwa Mkoa wa Kagera

Mafanikio katika Sekta ya Maji na Manufaa yaliyopatikana Mkoa wa Kagera yamefanikishwa na usimamizi mzuri wa viongozi wa sekta hiyo wakiongozwa na Waziri Jumaa Aweso na wasaidizi wake kwa kutekeleza maagizo ya Rais Dk. Samia anayowapa wakati wote.

Akielezea mafanikio hayo ya sekta ya maji Mkoa wa Kagera, Meneja wa RUWASA mkoa huo, Mhandisi Warioba Sanya alisema yapo maendeleo makubwa yaliyopatikana kipindi cha Rais Dk. Samia.

Alisema kumekuwepo ongezeko kubwa la asilimia za hupatikanaji wa huduma ya maji vijijini kutoka asilimia 70.06 mwaka 2020 hadi asilimia 83 machi 2025.

**Hadi kifikia Machi, 2025, jumla ya vijiji 560 kati ya vijiji 646, vinavyosimamiwa na RUWASA vina miradi ya maji ya bomba inayohudumia wakazi wapatao 2,500,531 sawa na asilimia 83 ya wakazi wote wa Mkoa wa Kagera wanaoishi maeneo ya vijijini**





WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJIJINI

*"Maji Bombani"*






# MAFANIKIO YA RUWASA MKOA KAGERA MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA

**Kutoka katika chanzo cha maji hadi ndani ya tanki, tayari kilomita 3.7 zimeshakamilika, huku mita 300 zikiwa katika hatua za mwisho. Tunajivunia hatua hii na tunatarajia kukamilisha kabla ya Oktoba mwaka huu**

"Kuongezeka kwa asilimia hizo kumesababishwa na kukamilika kwa miradi 44. Hii imeongeza muda kwa jamii kushughulikia mambo mengine ya kiuchumi katika jamii.

"Hadi kifikia Machi, 2025, jumla ya vijiji 560 kati ya vijiji 646, vinavyosimamiwa na RUWASA vina miradi ya maji ya bomba inayohudumia wakazi wapatao 2,500,531 sawa na asilimia 83 ya wakazi wote wa Mkoa wa Kagera wanaoishi maeneo ya vijijini," alisema.

**MAENEO AMBAYO HAYAJATEKELEZWA AU KUKAMILIKA**

Mhandisi Sanya alisema Pamoja na mafanikio hayo makubwa mkoani humo, bado RUWASA inakamilisha miradi ipatayo 15 katika maeneo ya Kaisho, Isingiro, Nkwenda, Runyinya Rwabwere hadi chanya, Kikukuru hadi Rubirizi, Rwanyango.

Alitaja maeneo mengine ni kimuli hadi Chakalisa wilaya ya Kyerwa, Katerere, Kumubuga, Ntanga na Nyamahwa wilaya ya Ngara.

Pia, Kigarama, Chaninika na Rugera wilaya ya Karagwe, Byeju, Kashenye hadi Mugana wilaya ya Missenyi, Bushagara, Migara, Katoro na Kaibanja wilaya ya Bukoba, Kyamyorwa hadi Rulanda, Kyabitembe, Katare hadi Buganguzi wilaya ya Muleba, Nyakahura, Katoke hadi Kalebezo wilaya ya Biharamulo.

Alisema ofisi ya chombo cha watoa huduma ngazi ya jamii kijiji Mushozi wilayani Bukoba.

**MIKAKATI YA UTEKELEZAJI WA MAENEO AMBAYO KUKAMILIKA**

Alisema RUWASA Mkoa Kagera umepanga kukamilisha miradi yote inayoendelea kwa kipindi kifupi kijacho walengwa wapate huduma lengwa kwa wakati sahii.

Alisema mikakati ya makusudi imewekwa kama kuwezesha vyombo vya watoa huduma ngazi ya jamii kusimamia miradi iliyokamilika na kuhakikisha inakuwa endelevu.

Alisema kuweka katika bajeti miradi itakayosaidia kutoa huduma maeneo ambayo bado hayajatekelezwa ikiwemo kubuni na kusanifu miradi maeneo ambayo bado hayajapata huduma ya maji fedha zinapopatikana kutekeleza miradi hiyo mara maja.

Serikali

Akielezea Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo Mathew, alisema kuwa Rais Dk. Samia, amebadili changamoto za maji kwa wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba Vijijini, mkoani Kagera, kuwa fursa kupitia ujenzi wa mradi mkubwa wa maji wa Kemondo-Maruku, ambao uko hatua za kukamilika.

Naibu Waziri Mathew alisema Dk. Samia, anapotekeleza miradi ya maji, anatatua kero za wananchi kwa kuzigeuza kuwa fursa za ajira, biashara na kuongeza mapato ya halmashauri.

"Rais Dk. Samia, anapotekeleza miradi ya maji anabadilisha changamoto kuwa fursa. Hii inatoa nafasi ya ajira, kukuza biashara na kuongeza mapato ya halmashauri zetu.

"Changamoto ya maji nchini inatatuliwa kwa vitendo na sasa wananchi wa Bukoba Vijijini watafaidika moja kwa moja," alisema Mathew.

Alisema mradi huo, mkubwa wa maji, unaogharimu sh. bilioni 15.8, umefanikiwa kufikia hatua ya juu baada ya zaidi ya sh. bilioni tisa kutolewa.

Alieleza kuwa, mradi unatarajiwa kunufaisha wakazi 100,000 wa kata sita kwa kuwapatia maji safi na salama.

"Kutoka katika chanzo cha maji hadi ndani ya tanki, tayari kilomita 3.7 zimeshakamilika, huku mita 300 zikiwa katika hatua za mwisho. Tunajivunia hatua hii na tunatarajia kukamilisha kabla ya Oktoba mwaka huu," aliongeza.

Naibu Waziri, Mathew alitoa wito kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi ya maji kuhakikisha vifaa wanavyotumia vinakidhi viwango vya ubora miradi hiyo iwe ya kudumu kwa muda mrefu.

Kwa upande wake, Katibu wa CCM wa Wilaya ya Bukoba Vijijini, Jesca Ndyamukama, alipongeza juhudi za Rais Dk. Samia na Wizara ya Maji kwa kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji nchini kwa ufanisi.

Naye Diwani wa Kata ya Kemondo, Hatwibu Mussa, alisema mradi huo ulianza mwaka 2021 kwa changamoto nyingi, lakini sasa unaonesha matumaini makubwa kwa wananchi.

"Tunamshukuru Rais Dk. Samia kwa juhudi zake. Mungu aendelee kumpa afya njema alete maendeleo zaidi," alisema Diwani Hatwibu.

**MRADI WA KEMONDO**

- Maruku ni miongoni mwa miradi mikubwa inayotekelezwa chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia kwa lengo la kuhakikisha kila mtanzania anapata Maji safi na salama hasa Vijijini.





**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA NISHATI**
**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA**

# TAARIFA YA MIRADI MIKUBWA YA UMEME INAYOTEKELEZWA KATIKA MKOA WA KAGERA



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan

Mkoa wa Kagera una jumla ya wilaya saba (7) ambazo ni Bukoba, Muleba, Biharamulo, Ngara, Missenyi, Karagwe na Kyerwa. Wilaya mbili (2) za Biharamulo na Ngara zinapata umeme kutoka kwenye Gridi ya Taifa kupitia kituo kipya cha kupoza umeme cha Nyakanazi kilichopo Wilaya ya Biharamulo. Wilaya tano (5) za Bukoba, Muleba, Missenyi, Karagwe na Kyerwa zinapata umeme kutoka Gridi ya Uganda. Wilaya za Bukoba na Muleba zinapata umeme kupitia kituo cha kupoza umeme cha Kibeta, na Wilaya za Karagwe, Missenyi na Kyerwa zinapata umeme kupitia kituo cha kupoza umeme cha Kyaka. Vituo hivi viwili vya Kyaka na Kibeta vinapokea umeme wa msongo wa Kilovolti 132 kutoka Gridi ya Uganda. Mahitaji ya juu ya umeme yaliyowahi kufikiwa kwa Mkoa wa Kagera ni MW 38. Kati ya mahitaji hayo, MW 31 zinatoka kwenye Gridi ya Uganda na MW 7 zinatoka kwenye Gridi ya Tanzania.







### HALI YA USAMBAZAJI UMEME KATIKA MKOA WA KAGERA

Hali ya usambazaji umeme katika Mkoa wa Kagera imeendelea kuimarika hasa kutokana na kuendelea kwa utekelezaji wa miradi kabambe ya usambazaji umeme vijijini inayofadhiliwa na Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA) pamoja na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), ambapo hadi kufikia mwezi Novemba 2024 jumla vijiji 658 kati ya vijiji 662 vimeshafikishiwa huduma ya umeme ambayo ni sawa na 99%.

### MIRADI MIKUBWA YA UMEME INAYOTEKELEZWA KATIKA MKOA WA KAGERA

### MRADI WA KUJENGA KITUO KIDOGO CHA UMEME (SWITCHING STATION) KATIKA WILAYA YA MULEBA

Faida ya Mradi: Mradi huu unalenga kuboresha upatikanaji wa umeme Wilaya ya Muleba. Kwa hivi sasa Wilaya yote ya Muleba inapata umeme kupitia laini moja tu ya umeme ambayo inatokea kwenye kituo cha kupoza umeme cha Kibeta kilichopo Bukoba. Hivyo, ikitokea hitilafu kwenye laini hiyo, wilaya yote ya Muleba inakosa huduma ya umeme.

Wigo wa Mradi: Mradi huo unahusisha ujenzi wa kituo kidogo (Switching Station) kwenye eneo la Ilemela wilayani Muleba, ujenzi wa laini ya kuunganisha kituo hicho (interconnector line) itakakayotokea kwenye kituo cha Kibeta na ujenzi wa laini tano za kutokea kwenye kituo hicho (outgoing feeders) ambazo ni laini za Kamachumu, Nshamba, Kyamuyorwa, Muleba mjini na laini ya kupeleka umeme kwenye kituo cha mafuta cha bomba la mafuta la Afrika Mashariki (EACOP) eneo la Kimea.

Gharama ya Mradi: Gharama ya mradi ni jumla ya Shilingi za kitanzania 8,451,364,483.28.

Hatua Iliyofikiwa Katika Utekelezaji wa Mradi: Kazi ya ujenzi wa laini ya kuunganisha kituo hicho (interconnector line) imekamilika kwa asilimia 98, usanifu (design) wa kituo kidogo umekamilika kwa asilimia 100 na kazi ya ujenzi wa laini ya kupeleka umeme kwenye kituo cha mafuta cha bomba la mafuta la Afrika Mashariki (EACOP) eneo la Kimea imekamilika kwa asilimia 66.5%.

Muda wa Kukamili kwa Mradi: Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni 2025.

### MRADI WA KUWEKA TANSFOMA YENYE UWEZO WA MVA 20 KWENYE KITUO CHA KYAKA

Faida ya Mradi: Mradi huu unalenga kuboresha upatikana wa umeme kwenye wilaya za Karagwe, Kyerwa na Missenyi, pamoja na mteja wetu mkubwa Kiwanda cha Sukari cha Kagera.

Wigo wa Mradi: Mradi huu unahusisha usafirishaji wa transfoma ya 20MVA kutoka kituo cha Mlandizi mkoani Pwani hadi Kyaka mkoani Kagera na ufungaji wa transfoma hiyo kwenye kituo cha Kyaka.

Gharama ya Mradi: Gharama ya kazi ya kusafirisha transfoma hiyo kutoka kituo cha Mlandizi mkoani Pwani hadi Kyaka mkoani Kagera pamoja na kuifunga

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA NISHATI**
**SHIRIKA LA UMEME TANZANIA**







# TAARIFA YA MIRADI MIKUBWA YA UMEME INAYOTEKELEZWA KATIKA MKOA WA KAGERA



transfoma hiyo kwenye kituo cha Kyaka ni Shilingi za kitanzania 400,000,000.00.

Hatua Iliyofikiwa Katika Utekelezaji wa Mradi: Mradi huu ulikamilika Mwishoni mwa mwezi Novemba 2024 baada ya kukamilika kwa majaribio ya transfoma iliyofungwa (trial run).

### MRADI WA KUJENGA KITUO KIKUBWA CHA KUPOZA UMEME ENEO LA BENACO NA UJENZI WA LAINI YA MSONGO WA KILOVOLTI 220 KUTOKA BENACO HADI KYAKA

Faida ya Mradi: Mradi huu unalenga kuziunganisha wilaya za Bukoba, Karagwe, Kyerwa, Missenyi na Muleba kwenye Gridi ya Taifa. Kwa sasa Wilaya hizo zinapata umeme kutokea kwenye Gridi ya Uganda.

Wigo wa Mradi: Mradi huu unahusisha ujenzi wa kituo cha umeme kwenye eneo la BENACO wilayani Ngara chenye uwezo wa MVA 80 (2 x 40MVA) pamoja na ujenzi wa laini ya usafirisha umeme ya msongo wa Kilovolti 220 kilomita 167 kutoka BENACO hadi KYAKA.

Muda wa mradi: Muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miezi ishirini na nne kuanzia Julai 2025.

Ufadhili wa Mradi: Mradi huu unafadhiliwa kwa ushirikiano kati ya Mfuko wa Maendeleo wa Abudhabi (Abudhabi Development Fund) ambao watatoa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 30, Mfuko wa Maendeleo ya Kimataifa wa OPEC (OPEC Fund for International Development) ambao watatoa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 60, Mfuko wa Maendeleo wa Saudi Arabia (Saudi Development Fund) ambao watatoa kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 13, pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itatoa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Bilioni 6.2.

Hatua Iliyofikiwa Katika Utekelezaji wa Mradi: Zabuni kwaajili ya kupata wakandarasi na kutekeleza mradi huo ilitangazwa tarehe 24/01/2025. Zabuni hiyo itafunguliwa tarehe 24/03/2025. Kikao cha utangulizi (Pre-bid meeting) kilifanyika Bukoba tarehe 17/02/2025 kikao hicho kilihusisha makampuni mbalimbali kutoka ndani na nje ya Tanzania ambayo yameomba kazi ya kutekeleza mradi huo.

### MRADI WA UPANUZI WA KITUO CHA KIBETA KILICHOPO MJINI BUKOBA

Faida ya Mradi: Mradi huu unalenga kuboresha upatikaji wa umeme kwenye wilaya za Bukoba (Mjini na Vijijini), Muleba na baadhi ya maeneo ya wilaya ya Missenyi kwa kuongeza uwezo wa kituo cha Kibeta kutoka MVA 20 za sasa (2x10MVA) hadi MVA 120 (2x60MVA)

Wigo wa Mradi: Mradi huu unahusisha uwekaji wa transfoma mbili zenye uwezo wa MVA 60 kila moja, ukarabati wa jengo la kuendesha kituo (Control Room) na ufungaji wa vifaa vipya vya kuendesha kituo (switch gears).

Gharama za Mradi: Mradi huu utagharimu jumla ya shilingi 14,779,288,272.95 za kitanzania.

Mkandarasi wa Mradi: Kampuni inayotekeleza mradi huu ni TBEA COMPANY LIMITED ya China.

Hatua Iliyofikiwa Katika Utekelezaji wa Mradi: Mkandarasi tayari yupo kwenye eneo la uwanda, na ujenzi wa misingi (foundations) kwa ajili ya kufunga vifaa husika unaendelea.

Mradi unatarajiwa kukamilika mwezi Mei 2025.

**MRADI**

***Faida ya Mradi: Mradi huu unalenga kuboresha upatikaji wa umeme kwenye wilaya za Bukoba (Mjini na Vijijini), Muleba na baadhi ya maeneo ya wilaya ya Missenyi kwa kuongeza uwezo wa kituo cha Kibeta kutoka MVA 20 za sasa (2x10MVA) hadi MVA 120 (2x60MVA)***



## WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI (TARURA) – MKOA WA KAGERA

# MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MATENEGENEZO YA BARABARA MIAKA MINNE YA RAIS. DR. SAMIA SULUHU HASSAN



Meneja wa TARURA mkoani Kagera, Wilson Charles

**UTANGULIZI**

TARURA Mkoa wa Kagera inahudumia Halmashauri nane (8). Halmashauri zinazohudumiwa na Wakala ni Biharamulo, Bukoba, Karagwe, Kyerwa, Missenyi, Ngara, Muleba na Manispaa ya Bukoba .

**MTANDAO WA BARABARA**

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Kagera una hudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya km 6,402.5, Madaraja 24, Kalvati 5135 na Madrifti 100.

**HALI YA BARABARA ZINAZOHUDUMIWA NA TARURA – KAGERA**

Hali ya barabara Mkoa wa Kagera imegawanyika katika makundi matatu, yaani zenye hali nzuri, zenye hali yakuridhisha na zile zilizoko katika hali isiyoridhisha kama ifuatavyo:-

1. Hali Nzuri Km. 1,510
2. Halia Kuridhisha Km. 3067.1
3. Hali Isiyoridhisha Km. 1,825.4.

**MAFANIKIO**

**Moja ya mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne ni kuongezeka kwa bajeti ya matengenezo ya barabara kutoka shilingi Bilioni 37.2 hadi shilingi Bilioni 110.3. Nyongeza hiyo ni sawa na asilimia 297 (297%). Ongezeko hili ni la kihistoria tangu kuanzishwa kwa Wakala huu mnamo mwaka 2017.**

**MAFANIKIO YA TARURA KWA KIPINDI CHA MIAKA MINNE YA AWAMU YA SITA YA RAIS, MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN**

Moja ya mafanikio makubwa yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka minne ni kuongezeka kwa bajeti ya matengenezo ya barabara kutoka shilingi Bilioni 37.2 hadi shilingi Bilioni 110.3. Nyongeza hiyo ni sawa na asilimia 297 (297%). Ongezeko hili ni la kihistoria tangu kuanzishwa kwa Wakala huu mnamo mwaka 2017.

Ongezeko hili linaashiria nia njema na halisi ya Rais, Mhe. Dr. Samia





Wilaya ya Kyerwa: Ufunguaji wa Barabara ya Nyaruzumbula- Kishanda B wakati wa ujenzi na ikiwa imekamilika kwa kutumia fedha za Jimbo. Hapakuwa na barabara kwani wananchi walitumia mitumbwi

# WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI (TARURA) – MKOA WA KAGERA

Suluhu Hassan ya kuleta maendeleo ya mwananchi mmoja mmoja na nchi kwa ujumla kupitia uboreshaji wa barabara za vijijini na mijini hapa Tanzania. Tunamshukuru sana.

Kupitia bajeti hiyo barabara, mafanikio makubwa yamepatikana kama ifuatavyo:-

- Barabara za Lami km 54.2 zimeongezeka kutoka km 81.3 hadi km 135.5 Sawa na asilimia 67%
- Barabara za Changarawe km 864.8 zimeongezeka kutoka km 1532.6 hadi km 2397.4 sawa na asilimia 56%
- Barabara za Udongo km 865 zimepungua kutoka km 4742 hadi km 3877 sawa na asilimia 18%

Aidha, ubora wa barabara umeongezeka kama inavyofafanuliwa hapa chini:-

- Barabara zenye hali NZURI km 347.8 zimeongezeka kutoka km. 1162.2 hadi km. 1510 sawa na asilimia 30% ya mtandao wa barabara,
- Barabara zenye hali ya WASTANI km 697.5 zimeongezeka kutoka km. 2369.5 hadi km. 3067 sawa na asilimia 29.5%
- Barabara zenye hali MBAYA km 746.2 zimepungua kutoka km. 2571.6 hadi km. 1825.4, sawa na 29%.

Mafanikio mengine yaliyopatikana ni:-



KYERWA

## TAARIFA YA MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA MATENEGENEZO YA BARABARA KWA MIAKA MINNE YA AWAMU YA SITA CHINI YA UONGOZI WA RAIS, MHE. DR. SAMIA SULUHU HASSAN KUANZIA MWAKA 2021/2022 – 2024/2025

- Ajira nyingi zimetolewa kupitia kazi za Makundi Maalum ya Wanawake, Wazee, Vijana na Wenye Ulemavu yaliyotekeleza Jumla ya Mikataba Nane (8) ya matengenezo ya barabara yenye thamani ya shilingi 736,763,760 katika maeneo mbalimbali hapa Mkoani Kagera
- Wakala umeboresha barabara nyingi ambazo zimemuwezesha mwananchi kufika kusikofikika na kuondoa vikwazo hasa maeneo yenye tingatinga kwa kujenga madaraja na miundombinu mingine.
- Hali ya usalama imeongezeka kwa kuwa maeneo mengi yanafikika.
- Kujenga barabara za lami katika makao makuu ya Wilaya, maeneo yenye vilima na maeneo yenye utelezi ili kurahisha usafiri na usafirishaji.

**AJIRA**

**Ajira nyingi zimetolewa kupitia kazi za Makundi Maalum ya Wanawake, Wazee, Vijana na Wenye Ulemavu yaliyotekeleza Jumla ya Mikataba Nane (8) ya matengenezo ya barabara yenye thamani ya shilingi 736,763,760 katika maeneo mbalimbali hapa Mkoani Kagera**



BIHARAMULO



BUKOBA

# KDCU inavyopaza sauti ya mkulima wa kahawa mkoani Kagera



**Na PHINIAS BASHAYA**

Chama cha Ushirika cha Wilaya za Karagwe na Kyerwa (KDCU)tangu kuanzishwa kwake mwaka 1990kimekuwa kimbilio la wakulima wa kahawa.

Kupitia chama hiki wakulima wameweza kuzikabili changamoto mbalimbali kwa umoja wao,huku wakinufaika na fursa mbalimbali ambazo zisiingefikiwa kama wasungekuwa katika jukwaa moja.

Wameweza kuyafikia masoko ya zao la kahawa kote duniani.Kupitia biashara hiyo wakulima wengi wa KDCU wana mengi ya kujivunia yatokanayo na nguvu ya umoja wao.

Baadhi yao wameboresha na kufungua mashamba mapya ya kahawa baada ya kuvutiwa na bei nzuri kwenye soko.Wengine wamefungua miradi ya kiuchumi na kuzalisha ajira kwa wengine.

Kupitia biashara ya kahawa,KDCU pia unachangia mamilioni ya fedha kwenye halmashauri za Wilaya ya Karagwe na Kyerwa,kutokana na kodi na ushuru unatokana na biashara yao.

Chama cha Wakulima wa Kahawa wa Wilaya za Karagwe na Kyerwa(KDCU) kimefanikiwa kupaza sauti ya wakulima ambao leo wanajivunia mafanikio mbalimbali

Baadhi ya mafanikio hayo ni uanzishaji wa i,miradi ya elimu na kumiliki mitambo ya kukoboa kahawa,ambavyo vyote kwa pamoja vinaongeza thamani ya jasho la wakulima wa kahawa.

**WANAMILIKI SHULE INAYOTIKISA KITAIFA**

Shule ya Sekondari Nyaishozi,kwa miaka ya karibuni imekuwa ndani ya orodha ya shule bora zinazofanya vizuri Kitaifa, katika mitihani ya kuhitimu kidato cha nne na sita.

Hii ni shule inayomolikiwa na wakulima wa kahawa,ambayo inahudumia wanafunzi kutoka katika makundi yote,kuanzia kwa wakulima,wafugaji na Watumishi wa umma.

Sifa za shule hii zinavuma kila Kona ya nchi hata kuwavutia wazazi na walezi kutoka Mikoa ya mbali.Mazingira bora na miundombinu imara ya shule hii vinaipa sifa ya ziada ya kuwa chaguo sahihi kwa mzazi kwa ajili ya elimu ya mtoto.

Shule ya Sekondari Nyaishozi yenye kidato cha kwanza hadi cha sita,inatoa unafuu mkubwa kwa wazazi wenye mdoto ya kuwaandalia watoto wao msingi mzuri wa elimu,utakaowasaidia kutimiza ndoto zao za kulitumikia Taifa kupitia fani mbalimbali.

**Sifa za shule hii zinavuma kila Kona ya nchi hata kuwavutia wazazi na walezi kutoka Mikoa ya mbali. Mazingira bora na miundombinu imara ya shule hii vinaipa sifa ya ziada ya kuwa chaguo sahihi kwa mzazi kwa ajili ya elimu ya mtoto.**

**WANAFUNZI WAUNGANA NA RAIS DK SAMIA SULUHU HASSAN**

Wanafunzi wa shule ya Sekondari Nyaishozi,kama wataalamu tarajiwa wa baadaye wamejenga shauku kubwa kwenye ajenda za Kitaifa zinazotajwa mara nyingi na Rais Dkt Samia Suluhu Hassan.

Wengi wao wanaguswa zaidi na ajenda ya Rais Samia ya kupikia debe matumizi ya nishati safi ya kupikia. Baadhi ya wanafunzi wa shule hii wanasema wao ni waathirika wa moja kwa moja wa matokeo ya athari za uharibifu wa mazingira.

Wanaijua namna ya kutetea ajenda hiyo,huku wakijenga hoja za kitaalamu kama zinavyoelezwa kupitia majukwaa mbalimbali yanayotoa elimu ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Mwaimukamu wa kipato cha nne Aneth Jackson anasema yeye kama mwanafunzi anayetamani mazingira salama kwa ajili ya kizazi chake na kijacho,yuko sambamba na ajenda ya



# KDCU inavyopaza sauti ya mkulima wa kahawa mkoani Kagera



Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

“Kama tukichona miti na kuharibu mazingira hatutapata mvua na nchi itakuwa jangwa, matumizi ya nishati safi yatapunguza adha ya kufuata kuni porini kwa watoto wa kike, nashauri gharama za kununua gesi zipungue Ili hata wananchi wa vijijini wanufaika” anasisitiza Aneth

Aidha mwanafunzi mwingine Elizabeth Castro kidato cha tatu,anasema matumizi ya nishati chafu ni chanzo cha baadhi ya wanawake kubebeshwa tuhuma za ushirikina hata kuuawa na wananchi.

Anasema kampeini ya Rais Dkt Samia inayoendelea sasa isambae hadi maeneo ya vijijini ambapo waathirika wengi wa matumizi ya nishati chafu wanapatikana ikilinganishwa na maeneo ya mijini.

Anasema mara kadhaa amemsikia Rais Dkt Samia akisisitiza umuhimu wa matumizi ya nishati safi kupitia vyombo vya habari.Anasema miti inapunguza hewa chafu na lazima ipandwe kwa wingi na kulindwa.

Maoni ya Stephen Muganyizi, mwanafunzi wa kidato cha tatu ni kumuomba Rais Samia awafikie hata wananchi wa vijijini ambao wanajitaji kuelimishwa zaidi kuhusu umuhimu wa matumizi ya nishati safi ya kupikia.

“Nampongeza Rais wangu Dkt Samia, kampeini yake inalenga kupunguza uharibifu wa mazingira,hata uchumi unaathirika kwa kuwa gharama kubwa zitatumika kutibu athari za kuharibika kwa mazingira”anaonya Muganyizi

### KAULI ZA WAKULIMA WA KAHAWA

Mashamba ya kahawa yamayotunzwa vizuri yanayomilikiwa na wakulima wanachama wa Ushirika wa KDCU,yanaonekana katika vijiji tofauti katika Wilaya za Karagwe na Kyerwa.

Baadhi yao wanasema Wanajivunia uimara wa Ushirika wao na sasa shauku ya kuongeza mashamba ya kahawa imeongezeka baada ya kuona mafanikio mbalimbali yaliyofikiwa.

Ili kukata kiu ya wanachama wake,KDCU imeanzisha programu ya Kusambaza bure miche bora ya kahawa. Ili kuchochea mafanikio zaidi,chama hicho kimeajiri maafisa ugani wanaotemnelea mashamba na kutoa ushauri kwa wakulima wanachama.

Miongoni mwa wakulima hao ni Datus Julius mkazi wa Kijiji cha Chanya, Kata ya Itera amayesema ameamua kufungua shamba jipya la kahawa baada ya kupata miche ya bure kutoka chama Chao cha Ushirika KDCU

Anasema kabla ya hapo pamoja na wakulima wengine walianza kukata tamaa kutokana na mwenendo usioridhisha wa bei ya kahawa katika masoko ya Kimataifa,hali iliyofanya waanze kufikiria mazao mengine mbadala ya biashara.

“Kwa sasa bei ya kahawa ipo juu, kupitia Ushirika wetu tunalipwa bei nzuri bila kuchelewa,tumepewa miche ya bure Ili tuongeze uzalishaji wa kahawa na maafisa ugani wanatutembelea kwa ajili ya kutusaidia na kutoa ushauri*anasema Julius

Naye mkulima wa Kijiji cha Muleba,Kata ya Itera Karimu Kassimu,anasema maafisa ugani wamesaidia kutatua changamoto,ambazo zilikuwa chanzo cha kupata mavuno habar hata kukata tamaa ya kuendeleza zao hilo. Anajivunia kwamba sasa bei ya kahawa imepanda akilinganisha na miaka michache iliyopita.

Chama cha Ushirika cha Wilaya za Karagwe na Kyerwa KDCU,kilianza rasmi mwaka 1990 baada ya kufikia makubaliano ya kujitenga na Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Kagera cha KCU 1990 LTD

Miongoni mwa mafanikio makubwa ya Ushirika huo,ni kufanikiwa kuwaunganisha wakulima wa Wilaya za Karagwe na Kyerwa,huku wakimiliki miradi mbalimbali ya kiuchumi kama hoteli,viwanda na shule katika Wilaya tofauti za Mkoa wa Kagera

**Kwa sasa bei ya kahawa ipo juu, kupitia Ushirika wetu tunalipwa bei nzuri bila kuchelewa, tumepewa miche ya bure Ili tuongeze uzalishaji wa kahawa na maafisa ugani wanatutembelea kwa ajili ya kutusaidia na kutoa ushauri**






# Wilaya ya Ngara yajivunia mafanikio miaka minne ya Rais Dk. Samia



Jengo la utawala makao makuu Halmashauri

**Na SUPERIUS ERNEST**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ngara ni miongoni mwa Halmashauri nane zilizopo Mkoa wa Kagera.

Halmashauri ipo Kaskazini Magharibi mwa Tanzania kati ya Latitudo 2° 45" Kusini na Longitudo 30°64" Mashariki

Ngara inapakana na nchi ya Rwanda kwa upande wa Kaskazini Magharibi na Burundi kwa upande wa Kusini Magharibi.

Kwa upande Mashariki inapakana na Wilaya ya Biharamulo, Kaskazini inapakana na Wilaya ya Karagwe,Kusini inapakana na Wilaya ya Kakonko Mkoa wa Kigoma.

Wilaya hii ina eneo la ukubwa wa kilomita za mraba 3,744, ambazo ni sawa na hekta 374,400.

Wilaya ya Ngara ina tarafa nne ambazo ni Nyamiaga, Kanazi, Rulenge na Murusagamba zinazounda Jimbo la Uchaguzi la Ngara.

Tarafa hizo zina jumla ya Kata 22, Vijiji 75, na Vitongoji 389, Mamlaka za mji mdogo 2 ambazo ni Ngara Mjini na Rulenge.

Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Wilaya ya Ngara, ina jumla ya watu 383,092, ambao kati ya hao 181,133 ni wanaume na 201,959 ni wanawake.



**Mkurugenzi Mtendaji Bw. Solomoni O. Kimilike**

**Katika kipindi cha miaka minne ya Awamu ya Sita ya Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imepata mafanikio makubwa ya maendeleo yaliyofanikishwa na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi(CCM).**

**UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA WILAYA YA NGARA**

Katika kipindi cha miaka minne ya Awamu ya Sita ya Serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara imepata mafanikio makubwa ya maendeleo yaliyofanikishwa na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi(CCM).

Wilaya hiyo imepokea kiasi cha sh. 51,895,541,915 ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali.

Sekta ya elimu ya awali na msingi sh. 8,516,063,115.00, sekta ya elimu ya sekondari, sh.15,810,865,334.00.

Katika Sekta afya serikali ilitoa sh.6,242,148,000.00, sekta ya kilimo, utawala na TASAF sh. 12,177,351,816.00, uwajibikaji kwa jamii (CSR) kupitia mradi wa uzalishaji umeme unaotekelezwa na nchi tatu ikiwemo Tanzania.

Mataifa mengine ni Rwanda na Burundi kiasi cha sh 9,149,113,650.00, Halmashauri imeendelea kupata hati safi kipindi cha miaka minne mfululizo kwa kufikia malengo ya fedha zinazotolewa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, unaishukuru na kuipongeza, serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia, kwa utekelezaji uliotukuka wa Ilani ya Uchaguzi wa Chama Cha Mapinduzi(CCM).

Ulisema serikali ya Rais Dk. Samia imefanya kazi kubwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo Ngara, haina budi kuipongeza kwa utendaji uliotukuka huku ukiahidi kuendelea kumuunga mkono kiongozi huyo wa **nchi kufanikisha malengo kusudia ya kuwaletea wananchi maendeleo.**



Shule mpya ya sekondari Mumurama kata ya Bukiriro

NHC
NATIONAL HOUSING CORPORATION
BUILDING OUR NATION



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) Hamad Abdallah

# NHC linavyojipambanua kupitia miradi yake mkoani Kagera



# NHC linavyojipambanua kupitia miradi yake mkoani Kagera

Na PHINIAS BASHAYA

Shirika la nyumba (NHC) katika uongozi wa Serikali ya awamu ya sita, limeendeleza mikakati yake ya kutoa huduma bora na nafuu kwa umma.

Kupitia uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano Dkt Samia Suluhu Hassan, shirika limeongeza kasi katika ujenzi wa makazi bora maeneo mbalimbali nchini.

Wananchi wananufaika na uwekezaji huo kwa njia tofauti, ikiwa ni pamoja na kujipatia makazi bora na nafuu, Kwa njia hiyo Shirika linawasaidia kuondokana na gharama kubwa za ujenzi wa makazi ya kisasa.

Juhudi za Shirika la nyumba nchini (NHC) zinakwenda sambamba na utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ambacho kilihaidi kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata makazi bora kwa gharama nafuu.

Wananchi wa Mkoa wa Kagera ni sehemu ya Watanzania, wananufaika na mipango ya uwekezaji unaofanywa na Shirika la nyumba, kupitia utekelezaji wa miradi yake mbalimbali.

### KITEGA UCHUMI MUTUKULA

Shirika la Nyumba nchini (NHC)limefanya uwekezaji mkubwa wa jengo la kitega uchumi katika mpaka wa Mutukula, Wilayani Missenyi unaotutenganisha na nchi jirani ya Uganda.

Jengo hili limeongeza taswira nzuri eneo la mpakani. Mazingira mazuri ya eneo hilo na miundombinu rafiki imevutia wafanyabiashara wengi kuendesha shughuli zao katika eneo hilo.

Meneja wa Shirika hilo Mkoa wa Kagera Deogratius Batakanwa, anasema jengo hilo la ghorofa moja limegharimu zaidi ya shilingi bilioni tatu.

"Wananchi waone jengo hili kama fursa ya kufanya biashara, nafasi bado zipo hata kwa wawekezaji kutoka nje baada ya kukamilisha taratibu zote zinazohitajika" anaeleza Batakanwa

Anasema mpaka sasa jengo hilo la kitega uchumi limepangishwa kwa asilimia sitini. Anatoa wito wa kutumia jengo hilo kufaidika na fursa za biashara mkoani.

Anazishauri hata Taasisi za kifedha kutumia jengo hilo kuweka mashine za kutokea fedha, huduma ambayo mahitaji yake yanaongezeka kila siku kutokana na kukua kwa biashara katika mpaka huo.

"Mradi huu ulibuniwa kwa ajili ya kuboresha mandhali ya mpaka na kuwa na eneo bora zaidi la kufanyia biashara, hata benki zinaweza kuanzisha "ATM zone" ndani ya jengo letu" anasema Meneja wa Shirika hilo.

Anasema Shirika la nyumba nchini linajivunia kuendelea kutoa huduma bora kwa umma. Pia kwa kushirikiana na sekta binafsi wametekeleza miradi mingi kwa ufanisi ambayo imekuwa



Meneja wa Shirika hilo, Mkoa wa Kagera, Deogratius Batakanwa

chanzo cha ajira kwa makundi mbalimbali.

Anataja miongoni mwa mafanikio ni kukuza taswira ya Shirika hasa majengo yenye hadhi ya Jiji, yanayojengwa kwenye maeneo ya Kata, kama kilivyo kitega Uchumi hicho kilichojengwa Kata ya Mutukula Wilayani Missenyi.

Kwamba kwa njia hiyo wamesisimua shughuli za uchumi hata kwa wananchi wa vijijini, huku Shirika likitengeneza nafasi za ajira za kudumu na zile za muda kupitia miradi yake mbalimbali.

Anasema Ili Shirika la Nyumba (NHC) iiendeleee kung'arisha maeneo ya mipakani hasa Mkoa wa Kagera kwa kuweka vitega uchumi linahitaji ardhi zaidi katika maeneo hayo.

Anatoa wito kwa halmashauri za Wilaya, kuwa na mipango ya kutoa ardhi kwa Shirika la Nyumba (NHC) kwa ajili ya uwekezaji wa miradi, ambayo kwa upande wa pili inawanufaisha wananchi.

'Halmashauri za Wilaya zianze kufikiria kutoa ardhi kwa ajili ya uwekezaji unaofanywa na Shirika la Nyumba, tunahitaji ardhi hata kwenye mipaka mingine" anaeleza Batakanwa

Kwamba kwa kuwa mahitaji ya huduma za Shirika la nyumba yanaongezeka kila siku, kwa mipango ya baadaye, watahitaji kuwa na ardhi katika miji midogo inayokua kwa kasi huku biashara zilishamiri katika maeneo hayo.

### GHOROFA JIPYA BUKOBA

Shirika la Nyumba (NHC) kupitia utekelezaji wa miradi yake, liko katika hatua za mwisho kuanzisha ujenzi wa jengo la ghorofa moja katika mji wa Bukoba barabara ya Kashozi.

Hatua ya Shirika hilo kuamua kuwekeza mradi huo wa zaidi ya bilioni moja, utakaokuwa na ghorofa moja ni kutaka kujibu mahitaji ya wananchi na wateja, wanaotafuta

## MAJENGO

**Matumizi ya mkaa ni kuchafua majengo kwa moshi,kuna uwezekano mkubwa wa kutokea kwa majanga ya moto na kusababisha madhara makunwa, tunatoa elimu kwa wateja wetu na kusisitiza watumie nishati safi' anasema Batakanwa**

maeneo bora ya kuendeshea biashara zao.

Meneja wa NHC Mkoa wa Kagera, Deogratius Batakanwa anasema wateja watakuwa na eneo bora la kufanyia biashara ndani ya Mwaka mmoja ujao. Maandalizi ya kuanza ujenzi wa kitega uchumi hicho tayari yamekamilika.

Pia jengo hilo kwa mipango ya baadaye, litakuwa na uwezo wa kuongezwa hadi kufikia ghorofa nne Ili kukidhi mahitaji ya wateja kwa wakati huo.

Shirika hilo linasema haliwezi kunyanyua ghorofa nyingi kwa sasa kwa kuwa miundombinu ya mji, lazima iboreshwe kwanza Ili iwe na uwezo wa kusafirisha maji taka kwa ufanisi tofauti na ilivyo sasa.

"Tunaandaa miradi kwa kuzingatia mahitaji ya wananchi, asilimia kubwa ya wateja wetu kwenye ardhi na majengo ni kutoka sekta binafsi,tunahakikisha huduma zetu zinakuwa bora" anasema Batakanwa

Anasema kupitia sera ya ubia, wanashirikiana na watu wengine katika biashara, huku akiwahamasisha wananchi kupanga katika majengo ya Shirika hilo kwa sababu ya ubora pia ni gharama nafuu.

### AJENDA YA NISHATI SAFI

Miradi ya Shirika la Nyumba (NHC) utekelezaji wake unazingatia kupaisha ajenda ya nishati safi ya kupikia ambayo inabebwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt Samia Suluhu Hassan hadi kwenye majukwaa ya Kimataifa.

Meneja wa Shirika hilo Mkoa wa Kagerra, Deogratius Batakanwa anasema ujenzi wa majengo yao mara zote unaacha nafasi, inayomuwezesha mteja kuunganisha nishati ya gesi kwa ajili ya matumizi yake.

"Matumizi ya mkaa ni kuchafua majengo kwa moshi, kuna uwezekano mkubwa wa kutokea kwa majanga ya moto na kusababisha madhara makunwa, tunatoa elimu kwa wateja wetu na kusisitiza watumie nishati safi 'anasema Batakanwa

Anashauri ajenda ya Rais Dkt Samia Suluhu Hassan, kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia inatakiwa kuungwa mkono na kila Mtanzania, kwa kuwa inalenga kuokoa mazingira. Itawaepusha wananchi na madhara yatokanayo na matumizi ya nishati chafu.

Pia anaipongeza Serikali kwa kuweka miundombinu inayohamasisha Uchumi wa kidijitali. Kwamba Shirika la Nyumba (NHC) pia ni wanufaika wa mipango hiyo, ambapo kwa kutumia mifumo ya kielektroniki qamefanikiwa kupunguza gharama.

Anasema kwa kutumia mifumo hiyo mteja anaweza kujihudumia bila ulazima wa kufika ofisini kama ilivyokuwa zamani.Imeondoa usumbufu na kuokoa muda wa wateja wa Shirika.

Shirika la Nyumba (NHC) limeendeleza kujipambanua kwa ubora wa huduma zake,. Ni Shirika la umma ambalo, wananchi wanapewa fursa ya kumiliki nyumba kwa gharama nafuu na kupanga kwenye majengo bora ya kuendeshea biashara.



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI
TANROADS



# TANROADS Kagera ilivyochochea maendeleo miaka minne ya Samia

## BILIONI 477.337

*Kujenga na kukarabati barabara kwa kiwango cha lami na kujenga madaraja*



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI
TANROADS

# TANROADS Kagera ilivyochochea maendeleo miaka minne ya Samia

## >>Yajenga barabara, madaraja kuchochea maendeleo na kukuza uchumi

Na SUPERIUS ERNEST

MAKALA ya Barabara (TANROADS) ni mojawapo ya taasisi zilizopo chini ya wizara ya ujenzi inayosimamia barabara kuu na za mikoa kuhakikisha zinakuwa katika hali nzuri na kupitika vizuri kipindi chote cha mwaka.

TANROADS Mkoa wa Kagera, wanahudumia jumla ya kilometa 2,076.25 za barabara. Kati ya hizo barabara kuu ni kilometa 861.57, barabara za mkoa ni kilometa 1,163.73 na za wilaya ni kilometa 50.95.

### HALI YA BARABARA KUU NA BARABARA ZA MKOA

Hali ya barabara zinazozisimamiwa na TANROADS zipo katika hali nzuri na wastani na zinapitika kipindi chote cha mwaka.

TANROADS Mkoa wa Kagera ilipokea fedha ya matengenezo ya barabara kuu na za mkoa zilizo chini ya wakala huo, ambapo ndani ya miaka minne, fedha za matengenezo ya barabara na miradi ya maendeleo zimeongezeka kutoka sh.Bilioni 18.990 kwa mwaka wa fedha 2021/22 kufikia wastani wa sh. Bilioni 19.467 kwa mwaka wa fedha 2024/25 sawa na asilimia 6.87



Muonekano wa daraja la Kitengule



Uchimbaji wa barabara katika mradi wa Bugene – Burigi – Chato unaoendelea



> Daraja hili limejengwa kwa lengo la kuunganisha miundombinu ya kiwanda cha sukari cha Kagera na barabara Kuu ya Kyaka, Bugene hadi Benako na barabara ya Kagera Sugar Junction hadi Kakunyu katika Wilaya za Missenyi na Karagwe.

### KUONGEZEKA KWA BARABARA ZA LAMI

Ujenzi wa barabara za lami umeongezeka kwa kilometa 25.7 kutoka kilometa 758.6 zilizokuepo mwaka 2021/22, kufikia kilometa 783.7 kwa mwaka 2024/25, sawa na ongezeko la asilimia 3.387.

### MIRADI MIKUBWA YA KIMKAKATI INAYOTEKELEZWA NA TANROADS MKOA WA KAGERA

Tanroads kwa kipindi cha miaka minne iliendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa ya maendeleo mkoani Kagera iliyo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Ujenzi wa Daraja la Kitengule lenye urefu wa mita 140 na barabara unganishi Kilometa 18

Daraja hili limejengwa kwa lengo la kuunganisha miundombinu ya kiwanda cha sukari cha Kagera na barabara Kuu ya Kyaka, Bugene hadi Benako na barabara ya Kagera Sugar Junction hadi Kakunyu katika Wilaya za Missenyi na Karagwe.

Mradi huu umejengwa kwa pesa za ndani kwa asilimia 84 na ushirika wa kiwanda cha Sukari Kagera kwa asilimia 16. Gharama ya mradi ni sh. bilioni 31.55,ambapo serikali imechangia Tsh. Bilioni 26.55 na uongozi wa kiwanda cha Sukari Kageraumechangia kiasi cha Tshs Bil 5.0.

Mradi ulianza oktoba 18, mwaka 2018 na kukamilika septemba, 2022 na sasa upo kwenye kipindi cha uangalizi.

### UJENZI WA BARABARA YA BUGENE – KASULO (BENACO) KM 60

Mradi wa Ujenzi wa barabara ya Bugene, Kasulo hadi Kumunazi kilometa 128.5, kipande cha Bugene - Burigi Chato kilometa 60 unatekelezwa na Mkandarasi aitwae M/s China Road and Bridge Cooperation (CRBC) ya China, thamani ya mradi ni Tsh. bilioni 92.84 bila kodi ya ongezeko la thamani.

Kazi ya Ujenzi ilianza mwezi Mei 10, mwaka 2022 na mradi unatarajiwa kumalizika April 10, mwaka 2026 ambapo kwa sasa kazi imefikia asilimia 42.

### MRADI WA UKARABATI WA BARABARA YA LUSAHUNGA – RUSUMO (KM 92) KWA KIWANGO CHA LAMI

Barabara hii ni moja kati ya mtandao wa barabara muhimu za Mkoa wa Kagera inayounganisha mkoa wa Kagera na Geita, kwa barabara kuu kupitia Kahama hadi Daraja la Rusumo na Rwanda, hivyo kuunganisha Tanzania na nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na DRC.

Mradi unatekelezwa na TANROADS chini ya Wizara ya Ujenzi kwa niaba ya Serikali.

Mkandarasi wa ujenzi ni M/S China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) akitekeleza kwa gharama ya Tsh. Bilioni 153.564, bila kodi ya ongezeko la thamani.

Mradi huo ulianza Julai 5, mwaka 2023 na unategemea kukamilika Disemba 10, mwaka 2026 kazi imefikia asilimia 24. Aidha,

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI
TANROADS

# TANROADS Kagera ilivyochochea maendeleo miaka minne ya Samia



Ujenzi wa Daraja katika mradi wa ukarabati wa barabara ya Rusumo-Lusahunga km 92

serikali imetoa kiasi cha Tsh. Bilioni 1.433 zilizotumika kulipa fidia kwa wananchi walioathiriwa na mradi huo.

**MRADI WA UJENZI WA BARABARA YA KAGERA SUGAR JUNCTION – KITENGULE JUNCTION (KM 25)**

Mradi huu unahusisha ujenzi wa barabara ya Kilometa 25 inayoanzia eneo la Bunazi kupitia kiwanda cha Kagera sugar hadi njia panda ya kitengule.

Mradi unatekelezwa na TANROADS chini ya wizara ya ujenzi kwa niaba ya serikali, ambapo mkandarasi ni M/S China Henan International Cooperation Group CO. LTD (CHICO) kutoka nchini China.

Gharama ya utekelezaji wa mradi ni sh. bilioni 54.79, bila kodi ya ongezeko la thamani ambapo muda wa utekelezaji ni miezi 24 ikiwemo miezi mitatu ya maandalizi. Utekelezaji wa mradi umeanza Tarehe Aprili 9, mwaka 2025 na unategemea kukamilika April 8, 2027.

Mkandarasi yupo eneo la kazi na tayari ameanza kazi za awali ikiwemo kazi ya kusafisha barabara. Aidha, jumla ya kiasi cha Tsh. Milioni 304.418 kimetolewa kwa ajili ya kulipa fidia na wananchi wote wanaostahili kulipwa tayari wamelipwa malipo yao ya fidia.

*Mradi unatekelezwa na TANROADS chini ya wizara ya ujenzi kwa niaba ya serikali, ambapo mkandarasi ni M/S China Henan International Cooperation Group CO. LTD (CHICO) kutoka nchini China.*

**UPANUZI WA NJIA NNE BARABARA YA BUKOBA BUKOBA PORT; KIPANDE CHA BUKOBA- HAMUGEMBE KILOMETA 1.0**

Mradi huu ulisanifiwa kwa ajili la suluhisho la kutatua tatizo la ajali nyingi zilizokua zikitokea kwenye mteremko na kona kali katika eneo la nyangoye. Mradi unahusisha upanuzi wa barabara hii kutoka njia mbili kuwa njia nne na pia kupunguza mteremko mkali kwenye eneo hilo.

Mkataba wa upanuzi wa barabara hii ulisainiwa September, 25 mwaka 2023. Mkandarasi wa mradi ni M/S Abemulo Contractors Co. Ltd ambaye anatekeleza kwa gharama Tsh. Bil 5.5. bila ongezeko la thamani.

Mpaka sasa utekelezaji umefikia asilimia 44, na kazi inategemea kukamilika Novemba 15, 2025. Aidha serikali imetoa jumla ya sh. Bilioni 1.87 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi walioathiriwa na mradi huu.

**UJENZI KWA KIWANGO CHA LAMI KWA BARABARA OMURUSHAKA-KAISHO- MURONGO; KIPANDE CHA KYERWA-OMURUSHAKA KM 50**

Mradi unatekelezwa kwa njia ya kusanifu na kujenga. Unasimamiwa na TANROADS na kutekelezwa na kampuni ya M/S Shandong Luqiao Group Co Ltd kwa gharama Tsh. Bil 94.093 bila ongezeko la thamani (VAT).

Muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miezi 36 kuanzia Juni 12 mwaka 2024 na utakamilika juni , 2027. Hadi sasa Mkandarasi yupo eneo la kazi akikamilisha kazi za awali kama usanifu wa barabara na madaraja na kujenga kambi ya msimamizi ili aweze kuanza kazi ya ujenzi.

**MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA MBALIMBALI ZA MANUNUZI**

Baadhi ya miradi iliyo kwenye hatua na manunuzi ni

Ujenzi wa Barabara ya Omugakorongo, Kigarama hadi Murongo Kilometa 111; Kipande cha Businde – Murongo( Kilometa 53.4), na

Ujenzi wa Barabara ya Kyaka, Katoro, Kanazi, Kyetema kilometa 60.7; Kipande cha Kanazi- Kalonge (kilometa 10).

**MIRADI MINGINE ILIYOKAMILIKA KUFANYIWA UPEMBUZI YAKINIFU NA USANIFU WA KINA**

Miradi ifuatayo tayari imekamilika kufanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina;-

- Ukarabati wa kilometa 29.11 za Barabara ya Mutukula hadi Kyaka kwa kiwango cha lami.
- Ujenzi wa barabara za Nyakahura- Kumubuga- Murusagamba, Keza- Rulenge, Murugarama na Rulenge- Kabanga Nickel (kilometa 141).

**MIRADI ILIYOPO KATIKA HATUA ZA USANIFU NA UANDAAJI WA NYARAKA ZA ZABUNI**

Upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka barabara ya Nyakahanga, Nyabionza hadi Nyakakika (kilometa 96) kwa kiwango cha lami unaendelea. Mtekelezaji wa mradi ni Mhandisi Mshauri, NIB-Plan Consults kwa gharama ya sh. milioni 554.965, Kazi hiyo ya usanifu imefikia asilimia 55. Miradi mingine iliyo kwenye hatua ya usanifu na upembuzi yakinifu ni:-

Upanuzi wa njia nne(4) wa barabara ya Magoti - Rwamishenyi-Kyakailabwa Km 6

Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Katoma- Bukwali (Kanyigo) Km 38

Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Magoti- Makonge -Maruku-Kanyangereko (Km 19.1)

Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Kigarama- Mabira -Kyerwa Km 50.95

Ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Rutenge-Rubare - Kishoju (Km 74)

Kufungua barabara ya mpakani ya Mutukula- Kakunyu (Km 56)

**UWEKAJI WA TAA ZA BARABARANI NA ZA KUONGOZEA MAGARI**

Ndani ya miaka minne ya serikali ya awamu ya sita, zimewekwa taa 618 za barabarani katika miji na barabara mbalimbali katika Mkoa wa Kagera kama ifuatavyo.

Wilaya ya Bukoba taa 230, Wilaya ya Muleba taa 46, Wilaya ya biharamulo taa 45, Wilaya ya Ngara taa 66, Wilaya ya Karagwe taa 165, Wilaya ya Keywa taa 42 na Wilaya ya Misenyi taa 25.

Vilevile, taa za kuongozea magari zimewekwa Bukoba mjini kwenye maeneo ya sido Hospitali ya Mkoa, na Rwamishenye.

**UJENZI WA MADARAJA MATANO YALIYOATHIRIWA NA MVUA ZA ELININO**

Kutokana na Mvua za Elinino zilizoanza kunyesha kuanzia mwezi Oktoba, 2023 hadi Mei, 2024 na kusababisha uharibifu wa baadhi ya madaraja, serikali ilipata fedha kutoka benki ya Dunia (WB) za ujenzi wa madaraja hayo yaliyoathiriwa na mvua hizo ambapo jumla ya madaraja matano yapo kwenye hatua mbalimbali za ujenzi. Madaraja hayo ni;-

- Daraja la Kanoni lenye mita 30; kazi imefikia asilimia 31
- Daraja la Kamishango lenye mita 45 kazi imefikia 50%
- Daraja la Kalebe lenye mita 60; kazi imefikia 30%
- Daraja la Kyanyabasa lenye urefu wa mita 105; kazi imefikia asilimia 25
- Daraja la Kyetema lenye mita 45; kazi imefikia asilimia 30



Upangaji wa mawe kwenye mitaro inayopitisha maji yanayotoka chini ya Ardhi





# MAFANIKIO YA MAMLAKA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA (BUWASA) MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN

Ndg. JOHN N. SIRATI
Mkurugezi Mtendaji



Ndg. Samora F.A Lyakurwa
Mwenyekiti wa Bod





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI
MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA

# BUWASA yaimarisha utendaji kazi miaka minne ya Rais Dk. Samia

## >>Yajivunia utoaji huduma bora kwa wananchi na utekelezaji miradi

**Na SUPERIUS ERNEST**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Bukoba (BUWASA), inahudumia Kata 14 zilizopo Manispaa ya Bukoba, kata tatu katika mji wa Kayanga/Omurushaka Wilaya ya Karagwe, kata tatu katika mji wa Kyaka/Bunazi wilaya ya Missenyi, kata sita katika wilaya ya Bukoba vijijini na kata moja katika wilaya ya Muleba.

Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama kwa eneo la Manispaa ni asilimia 93 na asilimia 84.8 kwa eneo lote la huduma ya Mamlaka ikiwafikia wananchi 339,639 kati ya wananchi 401,464 wote wanaohudumiwa na Mamlaka.

Akielezea hali na maendeleo ya BUWASA, Mkurugenzi Mtendaji, John Sirati alisema wanajumla ya wateja 30,149, ambao wanapata huduma za uhakika kutoka kwa Mamlaka hiyo..

Alisema Mamlaka kwa kutumia mapato ya ndani, imefanya upanuzi wa mtandao kwa kuwasogezea huduma ya maji wananchi walioko mbali na mtandao wa maji kwa kutumia fedha za ndani kiasi cha sh. 168,620,440.

Mkurugenzi Mtendaji Sirati, alisema maeneo yaliyofanyiwa upanuzi wa mtandao wa maji ni eneo la Ibosa, Kata ya Nyakato kilometa 2.5, kitongoji cha Kiwa kata ya Maruku kilometa tatu na kitongoji cha Bishonga kata ya Katoma kilometa 1.5.



**Mkurugenzi Sirati alisema Mwaka wa fedha 2024/2025, BUWASA inaendelea kutekeleza jumla ya miradi 11 kwa kutumia fedha za serikali yenye thamani ya sh. 18,969,718,143.38, ambapo miradi ya majisafi ni tisa yenye thamani ya sh. 15,891,301,493.38 na miradi ya usafi wa mazingira (majitaka) ni miwili yenye thamani ya sh. 3,078,416,650.0.**



### MIRADI INAYOENDELEA KUTEKELEZWA

Mkurugenzi Sirati alisema Mwaka wa fedha 2024/2025, BUWASA inaendelea kutekeleza jumla ya miradi 11 kwa kutumia fedha za serikali yenye thamani ya sh. 18,969,718,143.38, ambapo miradi ya majisafi ni tisa yenye thamani ya sh. 15,891,301,493.38 na miradi ya usafi wa mazingira (majitaka) ni miwili yenye thamani ya sh. 3,078,416,650.0.

Sirati alisema miradi yote 11 inatekelezwa kwa kutumia wakandarasi, ambapo jumla ya kiasi cha fedha zilizolipwa kwa utekelezaji wa miradi yote kufikia Desemba mwaka jana ni sh. 6,663,439,492.39 na kiasi cha fedha zinazohitajika kukamilisha miradi yote ni sh. 12,306,278,649.83.

Alisema Mamlaka kwa kushirikia na IFF-OBA Programme (Investment Financing Facility Output-Based Aid) kutoka Benki ya Maendeleo ya Ujerumani ( German Development Bank), inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kupunguza upotevu wa maji kwa kanda ya mjini katika kata za Bilele, Bakoba, Miembeni na Baadhi ya maeneo ya kata ya Hamugembe kwa ghrama ya sh. 1,365,710,149.

Sirati alisema mradi huo, unatekelezwa na mkandarasi Edonas Investment Limited Jv Rek One Co. Limited kwa mkataba No. TR154/2024/2025/W/01 kwa kipindi cha Muda wa



Mradi wa Maji Nyakasimbi-Karagwe DC

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAJI**
**MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA BUKOBA**





Mradi wa Maji Chanika –Karagwe Dc

# Mafanikio ya BUWASA Wilaya ya Bukoba miaka minne ya Rais Dk. Samia

miezi sita na utekelezaji wake ulianza Desemba 2024.

Vilevile, Mamlaka kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Kimkakati wa Miji 28 katika mji wa Kayanga Mradi wa maji Rwaka junju

"Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi M/S Afcons Infrastructure Limited and Vijeta Projects and Infrastructures Limited JV, gharama ya mradi ni dola za marekani milioni 27.963 sawa na sh. billioni 64.32, muda wa utekelezaji ni miezi 32, huku utekelezaji ulianza rasmi mwezi April 2023 na unategemea kukamilika ifikapo Desemba 2025, mradi umefikia asilimia 50.5 ya utekelezaji," alisema.

### UTEKELEZAJI MIRADI MIPYA 2024/2025

Mkurugenzi Mtendaji Sirati, alisema kwa Mwaka wa fedha 2024/2025, Mamlaka imepanga kutekeleza jumla ya miradi miwili kwa kutumia fedha za serikali yenye thamani ya sh. 2,140,236,993.43

### MPANGO WA UTEKELEZAJI MIRADI YA KIMKAKATI

Miradi ya kimkakati iliyopangwa kutekelezwa ni minne ambapo miradi ya maji ni mitatu katika mji wa Muleba, Buharamulo na Ngara na mradi wa ujenzi wa mtandao wa kuondoa maji taka Manispaa ya Bukoba.

Alisema usanifu wa miradi hiyo nyaraka zote muhimu za miradi imekamilika, kwa sasa wizara ipo katika hatua za kutafuta vyanzo vya pesa ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Alieleza kuwa, gharama za utekelezaji wa miradi hiyo ni sh. 191, 065,044,178 huku wanufaika ni 576, 795, ambapo utakuwa na tija kubwa kwa wananchi hao katika kupata huduma bora.

**Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi M/S Afcons Infrastructure Limited and Vijeta Projects and Infrastructures Limited JV, gharama ya mradi ni dola za marekani milioni 27.963 sawa na sh. billioni 64.32, muda wa utekelezaji ni miezi 32, huku utekelezaji ulianza rasmi mwezi April 2023 na unategemea kukamilika ifikapo Desemba 2025, mradi umefikia asilimia 50.5 ya utekelezaji**

### MAFANIKIO

Mkurugenzi Sirati alisema, wameongeza upatikanaji wa huduma ya maji kutoka asilimia 85 mwaka 2020 hadi asilimia 93 kwa mwaka 2024, kwa Manispaa ya Bukoba na kutoka asilimia 78 kwa mwaka 2022 hadi asilimia 84.8 kwa mwaka 2024 eneo lote linalohudumiwa na BUWASA.

"Kuongeza masaa ya huduma kutoka masaa 22 mwaka 2020 hadi masaa 24 mwaka 2024 kwa Manispaa ya Bukoba na kutoka masaa 20 kwa mwaka 2022 hadi masaa 22 kwa mwaka 2024 kwa eneo lote linahudumiwa na BUWASA.

"Kuongeza wateja kutoka 19,500 mwaka 2020 hadi 30,149 Desemba 2024, kuongeza makusanyo kutoka wastani wa milioni 250 kwa mwezi mwaka 2020 hadi milioni.474 kwa mwezi Desemba 2024, kujilipia umeme kwa asilimia 100,"alisema.

Pia, alisema kuongeza mtandao wa maji kutoka kilometa 376.7 mwaka 2020 hadi kilometa 719.8 Desemba 2024, kupandishwa daraja kutoka B kwenda daraja A kuanzia mwaka 2022, kuingia katika nafasi ya 10 bora katika utoaji wa taarifa ya huduma ya maji kwa wadau kwa Mamlaka za maji nchini, kufanikiwa kulipa masilahi ya watumishi kwa wakati ikiwemo makato ya kisheria.

### CHANGAMOTO

Mkurugenzi Sirati alitaja changamoto ni kuchelewa kwa upatikanaji wa fedha za utekelezaji wa miradi kutoka wizara ya maji, gharama kubwa za uzalishaji wa maji (Umeme na madawa ya kutibu maji), baadhi ya taasisi kutolipa madeni yake kwa wakati, upungufu wa maji kwa maeneo ya ukanda wa juu katika Manispaa ya Bukoba na maeneo ya mji wa Muleba na Kayanga, upotevu mkubwa wa maji upatao asilimia 35.3 kutokana na miundombinu chakavu.

### NAMNA YA KUKABILIANA NA CHANGAMOTO

Kuendelea na ufuatiliaji wa Fedha za utekelezaji wa miradi kutoka wizara ya maji, kuendelea na ufuatiliaji kwa kushirikiana na viongozi wa ngazi ya Mkoa na Kitaifa kwa malipo ya Madeni ya maji ya taasisi.

"Tumepata vibali vya kuboresha huduma ya maji kwa maeneo yenye changamoto ya upatikanaji wa maji katika mji wa Kayanga, Muleba, Mutukula na Ukanda wa Juu kwa Manispaa ya Bukoba. Tunaendelea na utekelezaji wa mradi wa kukabiliana na upotevu wa maji katika Mji wa Bukoba unaofadhiliwana IFF-OBA (KFW)










Mkuu wa Wilaya ya Bukoba Erasto Sima



Mkurugenzi halmashauri ya Bukoba Fatna Hussein



Mwenyekiti halmashauri ya Bukoba Murshid Ngeze

# DKT SAMIA SULUHU HASSAN ALIVYOPELEKA KAMPASI YA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM BUKOBA.




# DKT SAMIA SULUHU HASSAN ALIVYOPELEKA KAMPASI YA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM BUKOBA.



Mkuu wa Wilaya ya Bukoba Erasto Sima



Mwenyekiti halmashauri ya Bukoba Murshid Ngeze



Mkurugenzi halmashauri ya Bukoba Fatna Hussein

**Na Abel Shema.**

Ndoto ya Mkoa wa Kagera kuwa na kampasi ya kwanza ya Chuo Kikuu, itatimia hivi karibuni baada ya Serikali ya Awamu ya sita kutoa mamilioni ya fedha kwa ajili ya Ujenzi wa mradi huo wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mradi huu wa aina yake unaotekelezwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, (UDSM) kupitia Program ya Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya kiuchumi (HEET) unajengwa katika kijiji cha Itahwa, Kata ya Karabagaine Halmashauri ya wilaya Bukoba, kwenye eneo ekari 315.

Uamuzi huo wa Serikali ya Awamu ya sita, inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, unatimiza ndoto ya miaka mingi ya hitaji la kuwa na Vyuo Vikuu katika mkoa wa Kagera. Hiki kitakuwa ni Chuo Kikuu cha kwanza kuwa na kampasi yake katika Mkoa wa Kagera.

Kiasi cha shilingi bilioni 20 kinatarajiwa kutumika katika hatua za awali, huku wananchi wakionekana kuwa na hamasa kubwa ya kupokea mradi huo. Mradi umewezekana kutekelezwa katika halmashauri ya Wilaya ya Bukoba baada ya juhudi kubwa zilizofanywa na viongozi wa Wiaya hiyo,kuhakikisha ardhi kwa ajili ya mradi inapatikana.

Akizungumzia umuhimu wa mradi huo, Mkuu wa Mkoa wa Kagera Hajat Fatma Mwassa, anasema kampasi hiyo ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kitafungua fursa mbalimbali za uwekezaji na kuinua shughuli za uchumi wa wananchi.

Anasema kuwa pamoja na kuwa msaada mkubwa kwa mikoa mingine, pia kinafungua fursa kwa nchi nyingi jirani zinazopakana na Mkoa wa Kagera. Anamalizia wananchi waendelee kuonesha

**BILIONI 20**

**Kiasi cha shilingi bilioni 20 kinatarajiwa kutumika katika hatua za awali, hukuwananchi wakionekana kuwa na hamasa kubwa ya kupokea mradi huo. Mradi umewezekana kutekelezwa katika halmashauri ya Bukoba baada ya juhudi kubwa zilizofanywa na viongozi wa Wiaya hiyo, kuhakikisha ardhi kwa ajili ya mradi inapatikana.**

ushirikiano muda wote katika kipindi cha ujenzi huo na kwenye miradi nyingine ya maendeleo.

Anaongeza kuwa kwa sababu ya hulka ya wakazi wa Mkoa wa Kagera kupenda maendeleo ya Elimu, walisubiri ndoto hii itimie kwa miaka mingi, na jambo hilo limewezekana chini ya Uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika serikali ya Awamu ya sita.

Hii itakuwa Kampasi ya kwanza ya Chuo Kikuu kujengwa katika mkoa wa Kagera tangu Uhuru wa Tanganyika, huku Vyuo Vikuu vingine vikihamasishwa kufuata mkondo huo kwa kuwa kuna maeneo ya kutosha kufanya Ujenzi, wa miradi ya Taasisi za Elimu ya Juu.

**MIRADI ZAIDI YA ELIMU**

Nje ya Ujenzi wa Kampasi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) katika Halmashauri ya wilaya Bukoba pia Serikali ya Awamu ya sita imefanya uwekezaji mkubwa katika miradi mingine ya elimu kuanzia ngazi ya msingi hadi Sekondari.

Katika uongozi wa Serikali ya Awamu ya sita inayoongozwa na rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ipo miradi kinara inayotangaza mafanikio ya uboreshaji wa Sekta ya Elimu katika Halmashauri ya Bukoba. Baadhi ya shule zimejengewa miundombinu



Shule ya sekondari Katerero



ujenzi wa kampasi ya udsm Bukoba ukiendelea






Hospitali ya wilaya halmashauri ya wilaya ya bukoba

# Dkt Samia Suluhu Hassan alivyopeleka huduma za afya Bukoba.

imara na kurejea katika upya wake.

Ujenzi wa shule mpya 6 ambazo ni Shule ya Sekondari Rubafu,Katerero,Katoro,Butelankuzi,Mashule na shule ya msingi Kanaz B umechagiza ukuaji wa elimu ambapo miradi hii imekamilika na tayari wanafunzi wamejiunga na shule hizo

Ili kuimarisha usalama wa wanafunzi na mazingira bora ya shule, baadhi ya shule za Sekondari zimejengewa mabweni mapya na matundu ya vyoo ili kuondoa adha kwa wanafunzi na walimu. Mfano wa Sekondari hiyo ni Nyakato ambayo sasa imeng'arishwa upya kupitia mipango ya Serkali kuboresha elimu kuanzia ngazi ya msingi. Uboreshaji huu pia unakwenda sambamba na ujenzi wa nyumba za walimu.

Aidha shule ya msingi Kanazi 'B' inawakilisha shule zinazojivunia kuwa na majengo mapya ya utawala, madarasa mapya na ofisi za Walimu huku kiasi cha Shilingi milioni zaidi ya 540 zikitumika katika mradi huo.

**HOSPITALI YA WILAYA**

Miongoni mwa maeneo yaliyopewa kipaumbele na Serikali ya Awamu ya sita, chini ya Uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kuboresha huduma za Afya.

Imeongeza ujenzi wa Zahanati vituo vya Afya na Hospitali mpya na kufungua dirisha la ajira katika kada ya Afya.

**AFYA**

**Mradi huo umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 3, tayarI umeanza kuwanufaisha wananchi huku mipango ya Serikali ikiwa ni kuendelea kuboresha huduma za Afya**

Mradi huo umegharimu zaidi ya shilingi bilioni 3.2 tayari umeanza kuwanufaisha wananchi huku mipango ya Serikali ikiwa ni kuendelea kuboresha huduma za Afya kwa kuongeza wataalamu na vifaa tiba.Ili kusogeza huduma hizo karibu zaidi na wananchi.

Dhamira njema ya Serikali pia inaonekana katika ujenzi wa kituo cha Afya Rukoma. Kuna jengo la wagonjwa wa nje, nyumba za watumishi na jengo la wazazi ambalo linakidhi mahitaji ya wananchi.

Aidha Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba imepokea fedha kutoka Serikali Kuu ili zilizosaidia kuboresha huduma za upasuaji katika kituo cha afya Rubale.



# Tari inavyoimarisha usalama na uhakika wa chakula kupitia tafiti




## UTAFITI WA CHIKICHI NA PARACHICHI WALETA MATUMAINI

# Tari inavyoimarisha usalama na uhakika wa chakula kupitia tafiti



**NA PHINIAS BASHAYA**

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) imejikita katika tafiti zitakazoleta majibu ya kuwepo kwa uhakika na usalama wa chakula.

Miongoni mwa majukumu makubwa yanayoendelea kwenye vituo vya utafiti ni uhaulishaji wa teknolojia ambao umeleta mapinduzi ya kilimo.

Utafiti unaoendelea katika kituo cha TARI Maruku kilichopo Wilaya ya Bukoba,Mkoani Kagera,imekuwa mwanzo wa gunduzi nyingi za mbegu mpya zinazohimili magonjwa na kuongeza mavuno kwa mkulima.

Wataalamu wanaendelea kuzisafisha mbegu za asili kwa njia za kiteknolojia,Ili kupata mbegu safi zitakazokuwa na tija zaidi kwa mkulima.

Kwa sababu hiyo Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI)inajikuta inabeba dhamana kubwa ya kuhakikisha Taifa linakuwa na mbegu safi na salama kwa ajili ya uhakika wa chakula.

**MBEGU MPYA ZA MIGOMBA**

Wakulima wengi wa Mkoa wa Kagera,wanategemea Migomba ,kama zao lao kuu la chakula na biashara. Hata Uchumi wa Mkoa huo unategemea zaidi mafanikio kutoka kwa wakulima wa Migomba.

Hii ndiyo sababu hiki ni kituo kinachoongoza kwa tafiti za migomba hapa Watafiti wamefanikiwa kugundua aina mpya za migomba inayoweza kuhimili mashambilizi ya magonjwa na kipato cha mkulima.

Kuna mashamba manne yayayitumika kwa ajili ya utafiti wa aina mpya za migomba.Miongoni mwa mbegu mpya za migomba ni iliyopewa jina la TARIBAN.Mbegu hiyo inaanza na kizazi cha kwanza cha TARIBAN 1 na sasa imefika kizazi za nne na inafanya vizuri.

Kizazi cha nne cha TARIBAN kinatajwa na watafiti kwamba kina uwezo mkubwa wa kuvumilia ukame. Mbegu hii wanasema inafaa kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi. Hata hivyo hatua za mwisho za kiutafiti Bado zinaendelea,kabla mbegu hizo hazijarihusiwa rasmi kuwafikia wakulima baada ya kuthibitishwa na mamlaka nyingine inayohusika na udhibiti wa mbegu.

Wakulima wa Mkoa wa Kagera mashamba yao ya migomba yanashambuliwa na magonjwa kwa sababu mbalimbali. Miongoni mwa sababu zinazotajwa ni mazoea ya kubadilishana mbegu,hivyo kuwa chanzo cha kusambaa kwa magonjwa.

Kituo hicho tayari kina ekari 16 za mashamba ya mbegu safi,ambapo wakulima kwa makundi wanaendelea kunufaika na matokeo ya tafiti hizo kwa kujipatia mbegu bora na salama.

Pia Serikali imeendelea kuimarisha shughuli za utafiti katika kituo cha TARI Maruku,ambapo ujenzi wa maabara kubwa ya kuzalisha mbegu unaendelea.Maabara ikikamilika itakuwa na uwezo wa kuzalisha mbegu milioni tano ,ikilinganishwa na sasa ambapo Wana uwezo wa kuzalisha 1.5 milioni kwa mwaka.

Hii itakuwa miongoni mwa maabara kubwa Tanzania,itaongeza kasi ya uzalishaji wa mbegu na kukidhi mahitaji kwa wakulima waliolazimika kufuata mbegu bora nje ya Mkoa wa Kagera.

Pia itawapunguzia gharama za usafirishaji wa mbegu na kuepuka hasara waliyoipata baada ya mbegu kuharibika wakàti wa safari.

Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya kituo hiki kwa kuanza ujenzi wa ghala litakalohifadhi mbegu 35 milioni na litakuwa na chumba cha baridi kwa ajili ya kuhifadhi mbegu mama.

Aidha kwa kuwa shughuli za utafiti zinagharimu Serikali fedha nyingi,wataalamu wanasema ujenzi wa ukuta utazuia wizi wa majaribio ya kiutafiti. Wezi hufanikiwa kuingia kwa njia rahisi kwenye mashamba na kuiba mbegu au mazao ambavyo viko katika hatua mbalimbali za



TARI Transforming Agriculture




# Tari inavyoimarisha usalama na uhakika wa chakula kupitia tafiti



kiutafiti.

Ili kuendelea kufikisha elimu kwa wakulima,kituo cha TARI Maruku kimeanzisha mashamba darasa takribani ishirini katika maeneo mbalimbali kwa ajili ya mafunzo kwa wakulima,hasa wa migomba mipya iliyofanyiwa utafiti.

**UTAFITI WA CHIKICHI NA PARACHICHI WALETA MATUMAINI**

Mkoa wa Kagera sio maarufu sana kwa kilimo cha parachichi na chikichi. Hata hivyo tafiti za mbegu hizo zinazoendelea kituo cha TARI Maruku matokeo yake yameanza kuvutia wakulima.

Baadhi ya wakulima wanachukua mbegu katika vitalu vilivyopo katika kituo hiki na kuna mwitikio mkubwa kutoka kwa wakulima wa Wilaya za Ngara na Karagwe.

Kwamba mbegu zinazoandaliwa hapa zina uwezo wa kuhimili mazingira.Mbegu za parachichi zina ganda gumu hivyo kuwa na sifa ya kusafirishwa hadi masoko ya nje kibiashara.

Pia tatiti nyingine zinazoendelea kuwamufaisha wananchi ni mbegu bora za maharagwe.Uzalishaji wake gharama yake ni ndogo na watafiti wanasema wakulima wengi wanaweza kuzimudu.

Pamoja na kuwa na virutubisho vya kutosha mwilini pia mbegu hizo zina uwezo wa kukabiliana na mashambilizi ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mazao shambani.

Kupitia tafiti hizi za Kilimo,TARI inawezesha kufikiwa kwa mipango ya Serikali ya kuleta suruhisho la kipato kwa wananchii kupitia kilimo chenye tija,kinachozingatia matumizi ya mbegu bora na salama.

**TARI MARUKU IKO TAYARI KWA TATITI ZAIDI**

Mkuu wa Kituo cha Utafiti Maruku Dkt Mpoki Shimwela, anasema uwezeshaji unaofanywa na Serikali umesaidia kufikiwa kwa mafanikio yaliyopo na matarajio ni kuwa na tatiti nyingi zaidi.

"Wizara imeongeza fedha kwa ajili ya tafiti,tunafanya utafiti na ugunduzi tunasafisha Ili kupata mbegu safi na kutunza kizazi cha mbegu,tunataka wakulima wapande mbegu zisizo na magonjwa"anasema Dkt Mpoki

Pia anasema kituo hicho kinaongoza kwa tafiti za migomba hapa nchini na Mkoa wa Kagera unaathiriwa sana na magonjwa ya migomba hali inayoathiri uhakika wa chakula na kipato kwa wananchii.

Anasema Serikali imewezesha kituo kuwa na mashamba ya mbegu safi ekali 16,huku ujenzi wa maabara ya kisasa kwa ajili ya kuzalisha mbegu ukiwa katika hatua mbalimbali za ujenzi.

"Tunajenga maabara kwa ajili ya kuzalisha mbegu, mabaraza ikikamilika tutaweza kupata mbegu milioni tano kwa mwaka, leo tuna uwezo wa kuzalisha mbegu zisizozidi 1.5 miloni na itapunguza gharama za kusafirisha mbegu"anasema Dkt Mpoki

Anawashauri wakulima na wadau wa delta ya Kilimo kutumia mbegu bora zilizofanyiwa Utafiti na kuzalishwa na kituo hicho Ili waweze kupata matokeo bora wakati wa mavuno.

Pia anasema wataalamu wako tayari kutoa huduma kwa wakulima wanataka kupata matokeo makubwa zaidi na kituo hicho kinaendelea kupokea makundi ya watu mbalimbali wanaotemnelea mashamba kwa ajili ya mafunzo

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo



RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Biharamlo Mh. Leo Methew Rushahu





Bw. Innocent M. Mukandala, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Biharamulo



Advella Bulimba, Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo

# Bilioni 94.7 za Mhe. Rais Dk. Samia zilivyotua Wilaya ya BIHARAMULO




# Bil.94.7/= za Rais Dkt. Samia zilivyotua Wilaya ya Biharamulo



Advella Bulimba,
Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo



Mwenyekiti wa Halmashauri, Wilaya ya Biharamulo
Mh. Leo Methew Rushahu



Bw. Innocent M. Mukandala,
Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Biharamulo

**Na PHINIAS BASHAYA**

Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo Mkoani Kagera, imepokea kiasi cha shilingi bilioni 94.7 takribani kwa miaka minne kiasi hicho ni kile kilichopokelewa katika sekta zote Wilayani humo kwa ajili ya miradi ya wananchii na shughuli za maendeleo takribani kwa miaka minne ya uongozi wa Rais Dkt Samia.

Katika kipindi hicho, kiasi cha shilingi bilioni 52 zimepokelewa kupitia Halmashauri ya Wilaya hiyo na miradi mikubwa tofauti imetekelezwa na kukamilika na inawahudumia wananchii.

> ***Kwa upande wa shule za msingi, kiasi cha shilingi bilioni 13.7 zimetumika kuanzisha shule mpya na kufanya shule za msingi kuongezeka hadi 117 na shule shikizi mpya sita zikijengewa vyumba vipya.***



Wilaya ya Biharamulo inaongoza kwa wingi wa watu Mkoani Kagera wakifikia 457,114 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022,huku Mkoa ukiwa na jumla ya wakazi 2,989,299

Miradi mikubwa iliyotekelezwa ni katika sekta ya afya na elimu huku Wilaya hiyo ikifanikiwa kupandisha viwango vya ufaulu wa wanafunzi

Katika matokeo ya kidato cha nne mwaka 2024, Wilaya hiyo imeshika nafasi ya tatu, miongoni mwa Wilaya nane za Mkoa wa Kagera.

### TASWIRA MPYA KATIKA ELIMU

Mipango ya Serikali ya Awamu ya sita, kupitia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi(CCM)imewezesha Wilaya hiyo kutekeleza miradi mikubwa ya kuboresha elimu.

Baadhi ya shule mpya zimejengwa na Serikali na nyingine kuongezewa miundombinu ya vyumba vya madarasa,madawati na vyoo kwa ajili ya wanafunzi.

Juhudi hizi, zimekwenda sambamba kwenye shule za




# Bil. 94.7/- za Rais Dkt. Samia zilivyotua Wilaya ya Biharamulo



msingi na sekondari huku shule shikizi zilizoanzishwa kwa ajili ya kupunguza msongamano wa wanafunzi zikijengewa vyumba vipya vya madarasa.

Hatua hiyo imeongeza kasi ya kusudio la Serikali la kutaka kusogeza huduma karibu zaidi na wananchi wake. Hivyo imepunguza adha kwa wanafunzi ya kusafiri kwa umbali mrefu kufikia huduma za elimu

Kwa upande wa shule za msingi, kiasi cha shilingi bilioni 13.7 zimetumika kuanzisha shule mpya na kufanya shule za msingi kuongezeka hadi 117 na shule shikizi mpya sita zikijengewa vyumba vipya.

Kiasi cha shilingi bilioni 9.2 kiimetumika kuboresha miundombinu katika shule za sekondari huku shule mpya tisa zikiwa zimejengwa na kuanza kutumika na baadhi ya Kata zina shule tatu.

Shule mpya ya sekondari Kabindi pekee, imegharimu Serikali kiasi cha shilingi milioni 584 huku Wilaya ikiongeza ubunifu wa vyanzo vya mapato ili kuleta ufanisi zaidi katika huduma za wananchi.

**HUDUMA ZA AFYA ZIMEBORESHWA**

Miongoni mwa sekta zinazopewa umuhimu mkubwa na Serikali ni kuimarisha huduma za afya, hasa katika maeneo ya vijijini yenye changamoto kubwa zaidi za upatikanaji wa huduma hizo.

Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo,imefanikiwa kupiga hatua katika uboreshaji wa huduma hizo hivyo kupunguza baadhi ya changamoto zilizowakabili wananchi.

Imepunguza hatari ya vifo vya mama wajawazito na watoto kwa kuwa huduma zinapatikana karibu zaidi na maeneo yao.

Pia imepunguza uwezekano wa wananchi wagonjwa kukutana na hatari mbalimbali wakàti wa safari za kuelekea hospitali kwa ajili ya matibabu.

> ***Tutangaze mema ya Biharamulo, ni mengi sana, zaidi ya bilioni 94/- zimeletwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi katika uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia, hii ni kazi ya kupongezwa na hakuna sababu ya kulalamika***











# Bilioni 94.7 za Rais Dkt. Samia zilivyotua Wilaya ya Biharamulo

Kituo cha afya cha Bisibo kimejengwa kupitia utaratibu huo wa Serikali.Tayari kimepelekewa baadhi ya vifaa muhimu na wataalamu na wananchi wameanza kufurahia huduma.

Kwa mfano wananchi katika vijiji vya Kata ya Bisibo kabla ya huduma za afya kusogezwa,walisafiri umbali wa kilometa sita hadi tisa kufuata huduma za afya katika kituo cha Rukaragata.

Pia Serikali imekamilisha ujenzi wa hospitali ya Wilaya na vifaa muhimu huku kwa upande wa pili mafanikio hayo yakifungua dirisha la ajira kwa wataalamu wa kada mbalimbali.

**WANANCHI KUZIFIKIA FURSA**

Wilaya ya Biharamulo kupitia mipango yake mbalimbali,imewasaidia wananchi kuzifikia fursa mbalimbali ikiwa ni pamoja na biashara na masoko.

Wilaya ina wafugaji wengi wa nyuki,huku kwa muda mirefu wakivuna mazao mawili tu ya asali na nta badala ya mazao saba kama sumu ya nyuki na maziwa yake yenye thamani kubwa.

Ili waweze kuzifikia fursa hizo, baadhi ya wafugaji wa nyuki wamepewa mafunzo ya jinsi ya kuongeza thamani ya bidhaa zao,kupewa maeneo ya kufugia na elimu ya kuyafikia masoko.

Vikundi zaidi ya 25 vimenufaika na mipango hiyo ya Serikali kupitia Halmashauri yao ya Wilaya ya Biharamulo. Baadhi wameshiriki maonesho mbalimbali kwa ajili ya kujitangaza na kuzifikia fursa mpya kibiashara.

**WASEMAVYO WANANCHI**

Wananchi wa Wilaya ya Biharamulo ni wanufaika wa kwanza wa uboreshaji wa huduma na wanaijua tofauti ya kabla na baada ya miradi hiyo

> *Vikundi zaidi ya 25 vimenufaika. na mipango hiyo ya Serikali kupitia Halmashauri yao ya Wilaya ya Biharamulo. Baadhi wameshiriki maonesho mbalimbali kwa ajili ya kujitangaza na kuzifikia fursa mpya kibiashara.*






# Bilioni 94.7 za Rais Dkt. Samia zilivyotua Wilaya ya Biharamulo




kutekelezwa katika maeneo yao.

Baadhi ya wananchii wa vijiji vya Kata ya Bisibo, wanasema ujenzi wa kituo cha Afya katika Kata yao, imetatua changamoto nyingi ikiwa ni pamoja na kunusuru maisha ya wagonjwa waliosafiri mwendo mrefu kufuata huduma.

Miongoni mwa wanufaika hao ni Agness Anthony mkazi wa Kijiji cha Missenyi,Kata ya Bisibo, anasema adha ya kusafiri mwendo mirefu imepungua baada ya kujengwa kituo cha afya karibu.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Leo Rushahu anasema huduma nyingi zimesogezwa karibu zaidi na wananchi na matarajio ni kuimarisha mikakati ya kuongeza makusanyo ya ndani kupitia vyavzo mbalimbali.

**KAULI YA MKUU WA WILAYA**

Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo, Advella Bulimba, anasema Wilaya hiyo imepiga hatua kubwa baada ya kufanikisha miradi mbalimbali ya kuwahudumia wananchi,ikiwemo ya afya na elimu.

"Tutangaze mema ya Biharamulo ni mengi sana,zaidi ya bilioni 94 zimeletwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi katika uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt Samia hii ni kazi ya kupongezwa na hakuna sababu ya kulalamika" anasema Bulimba

Akitoa ufafanuzi wa kiasi hicho cha fedha,Mkuu huyo wa Wilaya anasema kiasi hicho ni jumla ya fedha iliyopitia katika sekta zote huku kiasi cha shilingi bilioni 52 zikiwa zimepita halmashauri ya Wilaya hiyo.

> ***Tutangaze mema ya Biharamulo ni mengi sana,zaidi ya bilioni 94 zimeletwa kwa ajili ya maendeleo ya wananchi katika uongozi wa Mheshimiwa Rais Dkt Samia hii ni kazi ya kupongezwa na hakuna sababu ya kulalamika***

**MKURUGENZI WA HALMASHAURI AFUNGUKA**

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Innocent Mukandala anasema changamoto nyingi zimepata ufumbuzi katika kipindi cha uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan na wananchi wanafurahia huduma ambazo awali hazikuwepo au zilikuwa mbali na wananchi.

"Katika kipindi cha uongozi wa awamu ya sita shule 31 mpya zimejengwa na kusajiliwa hadi kufikia jumla ya shule 117, shule shikizi sita zimejengewa madarasa mapya, kuna mabadiliko makubwa katika utoaji wa huduma kwa wananchii" anasema Mukandala

Anasema kuwa kiasi cha zaidi ya bilioni 52 zimepokelewa kwa ajili ya kuhudumia wananchii kupitia miradi mbalimbali katika kipindi cha uongozi wa Rais Dkt Samia Suluhu Hassan na baadhi ya changamoto zimepata ufumbuzi wa kudumu.

Anasema Wilaya hiyo Ina fursa nyingi kwa ajili ya uwekezaji wa miradi ya kiuchumi ukiwemo ufugaji wa nyuki na halmashauri Ina maeneo ya kutosha kwa ajili ya miradi hiyo.



Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Ofisi ya Raisi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
## Halmashauri ya Wilaya ya Muleba







Mkuu wa Wilaya ya Muleba,
Dr Alel Nyamahanga



Mwenyekiti wa Halmashauri,
Mhe. Magongo Justus John



Mkurugenzi wa Halmashauri,
Bw. Isaya Mugishagwe Mbenje

# UBORA WA MIRADI ULIVYOIFANYA MULEBA KUIBUKA MSHINDI WA KWANZA KITAIFA KIELLE CHA MBIO ZA MWENGE 2024




# UBORA WA MIRADI ULIVYOIFANYA MULEBA KUIBUKA MSHINDI WA KWANZA KITAIFA KIELLE CHA MBIO ZA MWENGE 2024


Mkuu wa Wilaya ya Muleba Dr Alel Nyamahanga


Mwenyekiti wa Halmashauri, Mhe. Magongo Justus John


Mkurugenzi wa Halmashauri, Bw. Isaya Mugishagwe Mbenje



**Na Phinias Bashaya**

Wilaya Muleba, Mkoani Kagera ndiyo kinara Kitaifa baada ya kutangazwa rasmi kwenye kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2024 zilzofanyika Jijini Mwanza.

Wilaya ya Muleba ilijitofautisha kwa ubora na upekee wa miradi ya maendeleo iliyokagulia au kuzindiliwa na kiongozi wa mbio za Mwenge mwaka 2024. Baadhi ya miradi hiyo iliwashangaza wakimbizza Mwenge kwa ubora na matokeo chanya kwa wanachi.

Hata ilipotangazwa kuwa mshindi wa kwanza Kitaifa, viongozi wa mbio za Mwenge na Waziri husika, waliweka wazi sababu za ushindi huo wa kwanza Kitaifa ambao huwaniwa kila mwaka na Halmshauri zote nchini.

Kupitia mbio za Mwenge viongozi kufanya tathmini ya thamani ya fedha, na jinsi viongozi na watendaji wa Halmashauri husika wanavyosimamia maelekezo na miongozo mbalimbali ya Serikali katika utekelezaji wa miradi.

Katika baadhi ya miradi wakati wa kilele cha mbio za Mwenge wa Uhuru jijini Mwanza, viongozi walitaja kuona matokeo ya kushangaza katika wilaya hiyo na kuwa sababu ya kupewa ushindi wa kwanza Kitaifa.

Tangu wakati hiyo miradi ya Halmashauri ya Wilaya ya Muleba inatumika kama shamba darasa kwa Wiaya nyingine. Baadhi ya viongozi wa Serikali wanaitaja baadhi ya miradi kama rejea katika hotuba zao mbalimbali.

Hata Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan katika moja ya hotuba zake, alitaja kuridhishwa na ubunifu wa mradi wa kilimo kwa vijana katika wilaya hiyo, kwamba ni mfano wa kuigwa.


Gharama za Mradi ni Shilingi 584,280,028
Shule iko kijiji cha Makongora, Kata ya Ruhanga
Shule hii itapunguza adha kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata masomo

Mradi huo wa vijana uliopo kata ya Nayondwe ambao vijana wanajiongezea kipato kupitia kilimo cha kisasa, baada ya kuwezeshwa ardhi na halmashauri yao pamoja na vitendea kazi, ndio ulikuwa na matokea makubwa yaliyowashangaza viongozi wa mbio za Mwenge.

Ni miongoni mwa Halmashauri chache nchini ambazo vijiji vyake bado vianamiliki ardhi, ambapo wakati wowote Serikali inaweza kuitumia kutekeleza miradi ya kiuchumi kama ilivyofanya kwenye mradi wa kilimo kwa vijana wa wilaya hii.

**HUDUMA BORA VISIWANI**

Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuwafikia wananchi wote huku ikiatatua vikwazo vilivyozuia kutufikiwa na huduma muhimu kama ukosefu wa barabara na vyombo vya usafiri. Wilaya ya Muleba inaundwa na baadhi ya visiwa kwenye ziwa Victoria. Wakazi wake pia wananufaika na mipango




> *Tangu wakati hiyo miradi ya Halmashauri ya Wilaya ya Muleba inatumika kama shamba darasa kwa Wiaya nyingine. Baadhi ya viongozi wa Serikali wanaitaja baadhi ya miradi kama rejea katika hotuba zao mbalimbali.*






# UBORA WA MIRADI ULIVYOIFANYA MULEBA KUIBUKA MSHINDI WA KWANZA KITAIFA KIELLE CHA MBIO ZA MWENGE 2024

mizuri ya Serikali yao pamoja na changamoto zilizopo kupitia mpango wa kuboresha huduma za Afya wa wananchi, Zaidi ya wakazi 15,000 kutoka kata tatu za visiwa vya Bumbire, hawalazimiki tena kufuata huduma nchi baada ya ujenzi wa kituo cha Afya Bumbire kukamilika.

Kabla ya hapo huduma zilipatikana maeneo mengine nje ya kisiwa hali iliyohatarisha maisha ya wagonjwa wakiwemo watoto na mama wajawazito. Sasa huduma zinapatikana kisiwani na mipango ya Serikali ni kununua boti za usafiri kwa ajili ya wananchi wake.

> *"Kabla ya hapo huduma zilipatikana maeneo mengine nje ya kisiwa hali iliyohatarisha maisha ya wagonjwa wakiwemo watoto na mama wajawazito. Sasa huduma zinapatikana kisiwani na mipango ya Serikali ni kununua boti za usafiri kwa ajili ya wananchi wake.*

Pia Wilaya inajenga mradi wa Jengo la dharura kituo cha Afya Kaigara (EMD) katika kijiji na Kata ya Muleba, ambapo lengo ni kupunguza vifo vitokanavyo na magonjwa mbalimbali.

Aidha hospitali ya Wilaya katika kijiji cha Marahala, Kata ya Magata inalenga kuhudumia wanachi Zaidi ya laki sita na kupunguza maradhi mbalimbali.

**SHULE MPYA ZIMEJENGWA**

Ili kutatua changamoto za kielimu, shule mpya zimejengwa na nyingine miundombuni yake ikiboreshwa ili kukidhi mahitaji ya walimu na wanafunzi. Mfano ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Biija itanufaisha wanafunzi 320, ambao walitembea umbali mrefu kufuata huduma za elimu. Zaidi ya Shilingi milioni 584 zimetumika katika mradi huu.

Aidha mradi wa shule mpya ya Amali Mubunda umejengwa lengo la Serikali ikiwa ni kupungua changamoto mbalimbali ikiwemo kusafiri umbali mrefu, ambapo hatua hiyo pia inatarajiwa itapandisha viwango vya ufaulu wa wanafunzi.

Mkurugenzi wa halmashauri hiyo Issaya Mbenje, anasema miradi mingi imetatua changamoto na kuongeza ufanisi wa shughuli za uchumi na kijamii.

Anatoa mfano wa shule ya sekondari Makongola ni miaongoni mwa shule bora iliyojengwa kikamilifu. Mradi huo ulipongezwa na Kiongozi wa mbio za mwenge wa Uhuru mwaka 2024 na kutajwa kama mfano wa miradi borailiyotoa taswira ya thamani ya fedha zilizotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita

Anasema gharama za Mradi ni Shilingi 584,280,028 na imejengwa katika Kijiji cha Makongola,Kata ya Ruhanga.Shule hii itapunguza adha kwa wanafunzi kutembea umbali mrefu kufuata masomo







# Wilaya ya Kyerwa inavyong'aa kwa miradi lukuki ya maendeleo











Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa,
Mhe. Zaituni Msofe



Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa,
James John






# Wilaya ya Kyerwa inavyong'aa kwa miradi lukuki ya maendeleo



Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, Mhe. Zaituni Msofe



Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa, James John

## >>Wampongeza Rais Dk. Samia kwa kasi ya maendele yaliyopatikana kwa miaka minne

**Na PHINIAS BASHAYA**

Wilaya ya Kyerwa, iliyoko mkoani Kagera inajitofautisha kutokana na hali yake nzuri ya hewa na rutuba nzuri ya shughuli za kilimo cha mazao ya chakula na biashara.

Ni miongoni mwawilaya chache nchini ambazo zinapakana na nchi zaidi ya moja.

Kwa upande wa Kaskazini inapakana na nchi ya Uganda, Magharibi inapakana na Rwanda ikitenganishwa na mkondo wa mto Kagera.

Umbali kati ya halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa na Jiji la Dar es salaam ni kilometa 1,880. Umbali kati ya Wilaya hiyo na Makao Makuu ya Mkoa yaliyopo Bukoba Mjini ni kilometa 195

Shughuli kubwà za kiuchumi ni ufugaji na kilimo cha mazao ya biashara hasa kahawa. Ardhi inaruhusu kilimo cha mazao ya chakula kama ndizi na mazao ya mizizi, hivyo wananchi wengi kuwa na uhakika wa chakula kwa kipindi chote cha mwaka.

Jengo la kisisa la utawala ni kielelezo cha jitihada za serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuboresha miundombinu ya kazi kwa watumishi.

Mazingira salama ya kazi ni kichocheo cha ufanisi wa kazi kwa watumishi kuwawezesha kutoa matokeo chanya na tarajiwa kuakisi maono ya viongozi wa serikali.

**MIRADI YA MAENDELEO**

Miradi ya maendeleo imegusa sekta zote, ambapo wananchi katika vijiji mbalimbali wanatoa ushuhuda wa mabadiliko chanya yaliyopo sasa kulinganisha na miaka minne iliyopita.

Sera za Serikali ya Awamu ya Sita,inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kuhusu uboreshaji wa huduma za afya, imekuwa sababu ya ujenzi wa vituo vipya vya afya na hospitali ya Wilaya.

Kabla ya hapo, wananchi wa Wilaya ya Kyerwa walifuata huduma za vipimo vikubwa na matibabu nje ya wilaya hiyo.

Kwa hivi sasa, huduma nyingi za matibabu na vipimo vinapatikana ndani ya Wilaya hiyo, hivyo kuwapunguzia changamoto ya kusafiri umbali mrefu na kupunguza gharama.

Mradi wa maji wa Kagenyi-Omukilinzi ni miongoni mwa miradi ya hivi karibuni iliyobuniwa kuondoa kero kwa wananchi.

Ubora wake unawakilisha taswira ya juhudi za Serikali ya Rais Dk. Samia, inavyopambana kusogeza huduma hizo karibu na wananchi.

Mradi huo umejengwa kupitia fedha za mipango ya lipa kwa matokeo, lengo la serikali ni kuwasaidia wananchi kupata huduma ya maji kwa umbali usiozidi mita mia nne.

> **MAFANIKIO**
>
> **Kabla ya hapo Wananchi wa Wilaya hii walifuata huduma za vipimo vikubwa na matibabu nje ya Wilaya hiyo Hivi sasa huduma nyingi za matibabu na vipimo vinapatikana ndani ya Wilaya hiyo, hivyo kuwapunguzia adha ya kusafiri mwendo mrefu na kupunguza gharama.**

Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji Vijijini Wilaya ya Kyerwa (RUWASA) Kashonele Kagodoro, alisema lengo la mradi huo ni kusaidia wananchi kupata huduma ya maji safi na salama maeneo ya karibu.

"Lengo la mradi huu kupitia fedha za program ya lipa kwa matokeo ni kusaidia wananchii kupata huduma ya maji kwa wepesi, umbali usiozidi mita 400 na tumepeleka umeme katika chanzo"alisema Kagodoro

Pia, alisema pamoja na miradi ya maji kuanzishwa kwa ajili ya kuwasaidia wananchi, taasisi mbalimbali ikiwemo zahanati na shule ni wanufaika wa miradi hiyo.

"Miradi hii itawasaidia wananchi kupata muda wa kutosha kufanya shughuli za uzalishaji na kujiongezea kipato, wataokoa muda walitumia kusafiri umbali mrefu kufuata huduma ya maji, hata taasisi za shule na zahanati zinafaidika na miradi hii"alisema

Alisema ujenzi wa mradi huo, ni mkombozi mkubwa kwa wananchi wa vijiji mbalimbali ambao ili kuunga mkono juhudi za serikali yao walichangia sh. 1,200,000, ambapo mradi huo uligharimu sh. 261,200,000.00.

Kuhusu uboreshaji wa mazingira ya elimu katika Wilaya ya Kyerwa, alisema ni taswira inayoonekana wazi maeneo mbalimbali hususan ujenzi wa shule mpya kuanzia za awali hadi za sekondari.

Alieleza kuwa, kupitia mradi wa SWASH(S.R.WSS)shule nyingi










# Wilaya ya Kyerwa inavyong'aa kwa miradi lukuki ya maendeleo

zimekarabatiwa na miundombinu kuimarishwa upya, ambapo shule za msingi Mkapa na Rwensinga ni mfano mzuri wa mafanikio hayo.

MRADI WA PIKIPIKI KWA VIJANA

Ili kwenda sambamba na mahitaji ya vijana, Halmashauri ya Wilaya ya Kyerwa imebuni mipango mbalimbali ya kuunga mkono juhudi za makundi ya vijana wenye dhamira ya kujikwamua kiuchumi kupitia shughuli mbalimbali.

Alisema halmashauri imewafikia vijana hao kupitia makundi yaliyotambuliwa na kusajiliwa kwa mujibu wa taratibu, ikiwani ni hatua muhimu ya kuwezesha vikundi kunufaika na fursa mbalimbali zinazotolewa na serikali.

Kikundi cha waendesha pikipiki kinatumika kama mfano bora wa aina ya makundi ya vijana, wanaonufaika na fedha zinazotokana na mkopo wa asilimia kumi unaotolewa na halmashauri hiyo.

Baada ya vijana hao kupata mkopo wa pikipiki kumi na nne,wameimarisha shughuli zao za usafirishaji katika Kata za Nkwenda, Rukulaijo na Kitwechenkura.

Alisema vijana hao sasa wana uhakika wa kipato kupitia shughuli zao za kujiajiri katika usafirishaji wa abiria kwa kutumia pikipiki.

Kiongozi wa kikundi hicho Erick Kazinja, alisema walianza mwaka 2018 na baada ya kufanya usajili wamepata sifa ya kunufaika na fedha zitokanazo na mkopo wa asilimia kumi kutoka halmashauri yao.

Alisema baada ya kupata mkopo wa milioni 26,walinunua pikipiki na kujiajiri katika usafirishaji wa abiria, huku akiwahamasisha vijana kujiunga katika vikundi wanufaike na fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia.

**TAARIFA YA MKUU WA WILAYA**

Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, Zaitun Msofe, alisema kupitia mikutano na wananchi amekuwa akifafanua mafanikio yaliyofikiwa na umuhimu wa kuendelea kuunga mkono jitihada za serikali zinazolenga kuwaletea wananchi maendeleo.

Katika hotuba yake kupitia sherehe za siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, zilizofanyika April 26, mwaka huu, Mkuu wa wilaya Zaituni aliwakumbusha wananchi wingi wa miradi ya maendeleo na kuwataka kulinda na kuithamini.

> **VIJANA**
>
> **Halmashauri imewafikia vijana hao kupitia makundi yaliyotambuliwa na kusajiliwa kwa mujibu wa taratibu,ambapo hii ni hatua muhimu ya kuwezesha vikundi kunufaika na fursa mbalimbali zinazotolewa na Serikali yao.**

"Zaidi ya asilimia tisini tumezaliwa ndani ya Muungano,tutangulize kwanza masrahi ya Taifa, tuendelee kufundishana na kuelimishana huku tukiulinda Muungano wetu"alisema Zaituni.

Aliwataka wananchii kulinda umoja na amani kwa wivu mkubwa, huku wakiungana na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk. Samia katika jitihada zake za kuwaletea maendeleo.

Aliwataka Wananchi wa Wilaya hiyo ya Kyerwa, kujiandaa na Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Octoba, Mwaka huu, wajitokeze kujiandikisha,kuhakiki taarifa zao kujitokeza kupiga kura.












**Mbunge Wa Missenyi Florent Kyombo**



**Mheshimiwa mkuu wa Wilaya canal mstaafu Hamis Maiga Mayamba**



**Mwenyekiti wa Halmashauri, Projestus Tegamaisho**



**Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Bw. John Paul Wanga**

**Mwonekano wa soko la Bunazi kwa sasa**



**Mwonekano wa soko la Bunazi kwa siku zijazo**



# Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi yajipambanua na mafanikio lukuki




# Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi yajipambanua na mafanikio lukuki



Ujenzi wa nyumba ya walimu Kitobo Sekondari



HOSPITALI YA HALMASHAURI YA WILAYA

**Na SUPERIUS ERNEST**

MIAKA minne ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imechochea maendeleo makubwa katika wilaya, Halmashauri na Mikoa.

Halmashauri ya Wilaya ya Misenyi, ni miongoni mwa zile zilizoguswa na mafanikio hayo makubwa katika kipindi cha miaka minne ya Rais Dk. Samia.

Akielezea mafanikio hayo, Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi, John Wanga alisema katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Dk. Samia, Wilaya ya Missenyi inajivunia mafanikio mengi hususan huduma za jamii, kiuchumi, uzalishaji, mawasilino na usafirishaji.

**ELIMU MSINGI**

Alisema Wilaya ya Missenyi inajivunia kupokea Tsh. 8,151,098,521.25 ikiwa ni elimu bila malipo ni Tsh 4,169,898,521.25, na Tsh 3,981,200 ni miundombinu ambapo vimejengwa vyumba vya madarasa 142, kuongezeka kutoka vyumba 643 kwa mwaka 2020 hadi 785 kwa mwaka 2025.

Alisema nyumba za walimu sita zimejengwa, kuongeza idadi ya nyumba za walimu kutoka 209 mwaka 2020 hadi 2015 kwa mwaka 2025, matundu ya vyoo 392, yamejengwa hivyo kuongeza idadi kutoka 1,087 kwa mwaka 2020 hadi 1479 kwa mwaka 2025.

"Mafanikio mengine ni ufaulu wa darasa la saba umeongezeka kutoka asilimia 82 hadi asilimia 85. Uandikishaji darasa la awali na darasa la kwanza umeongezeka kwa asilimia 18.

"Idadi ya walimu kutoka 154 mwaka 2020 hadi 733 mwaka 2025. Ongezeko la shule saba za msingi ambazo ni Kafunjo, Muungano, Itara, Bunazi B, Kabwera, Bwenkoma na Kitoboka, kufanya jumla ya shule za serikali kuwa 103 kwa mwaka 2025 kutoka shule 96 kwa mwaka 2020 na ujenzi wa shule mpya ya bunazi,"alisema.

**ELIMU SEKONDARI**

Alisema elimu ya sekondari, kwa kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka 2020/2021, Halmashauri imepokea sh. 10,138,531,000.28, ikihusisha fedha za elimu bila malipo sh. 3,058,898,000.57, ikiwa ni ongezeko la sh 1,710,428,000.58 ukilinganisha na mwaka 2021 na sh. 7,070,633,317.73 ya uboreshaji wa miundombinu.

Alieleza kuwa, jumla vyumba vya madarasa 388 vimejengwa ikiwa ni ongezeko la vyumba 118 ukilinganisha na vyumba 270, vilivyokuwepo mwaka 2021.

"Kwa kipindi cha miaka mitano halmashauri imejenga maabara 29 hivi kufikisha mabara 77 sawa na asilimia 100 zilizojengwa katika shule za sekondari" alieleza Mkurugenzi Wanga.

Alieleza kuwa, Matundu ya vyoo 460 yamejengwa ikiwa ni ongezeko la matundu 125 ya mwaka 202. Ujenzi wa nyumba ya walimu Kitobo sekondari.

**Maabara zilizojengwa ni 75, ongezeko la maabara 29 zilizokuwepo Mwaka 2025. Jumla ya nyumba za walimu tatu zenye uwezo wa kuishi familia mbili, kila moja zimejengwa shule ya Bugando, Kitobo na Bunazi.**

**SEKTA YA AFYA**

Mkurugenzi Mtendaji Wanga alisema kwa kipindi cha miaka minne wamepokea fedha kutoka Serikali kuu Sh 9,385,327,435.88 kati ya fedha hizo Sh 3,250,381,549.88 ni za vifaa tiba na Dawa na Sh 6,134,945,886.00 za miundombinu.

Alisema jumla ya zahanati zilizojengwa ni 7 hivyo kuongeza idadi ya zahanati kutoka 25 mwaka 2020 hadi 32 mwaka 2025.Vituo viwili vya Afya vimejengwa na hivyo kuongeza idadi ya vituo vya Afya kutoka vinne kwa mwaka 2020 hadi sita kwa mwaka 2025. Nyumba tatu za watumishi wa Afya zimejengwa na kuongeza idadi kutoka nyumba 79 kwa mwaka 2020 hadi nyumba 82 kwa mwaka 2025.

Historia imeandikwa katika Wilaya ya Missenyi , Halmashauri haikuwa na Hospitali ya Wilaya lakini kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025 imejengwa Hospitali Mpya.

Alitaja mafanikio mengine ni kupatikana kwa dawa kutoka asilimia 93 kwa mwaka 2020 hadi asilimia 98 mwaka 2025, huku huduma za upasuaji zimeanza kutolewa katika kituo cha Afya Bunazi na Hospitali ya Wilaya baada ya kupokea wataalamu na vifaa tiba vya kisasa.Aidha magari ya kubebea Wagonjwa yameongezeka kutoka magari 2 hadi magari 5 kwa sasa.

**HUDUMA YA MAJI MJINI NA VIJIJINI**

Alisema serikali imeongeza kasi ya kumtua mama ndoo kichwani ambapo kwa kipindi cha miaka minne sh. 10,167,123,737.31 zimetolewa kujenga miradi ya maji 11 kutoka miradi tisa ya mwaka 2020 hadi miradi 18 maeneo ya Missenyi.

Alieleza kuwa, miradi hiyo imechangia asilimia ya upatikanaji wa maji kutoka asilimia 58 kwa mwaka 2020 kwa mjini kufikia asilimia 78 kwa mwaka 2025 kwa vijiji.

Mkurugenzi Wanga alisema idadi ya watu wanaopata maji safi na salama ni 191,407 sawa na asilimia 78 ya wakazi wa Missenyi ikiwa ni ongezeko la asilimia 20 katika kutaja gharama za miradi ikiwemo ya BUWASA.

**HUDUMA ZA KIUCHUMI**
**3.1 KILIMO/MIFUGO NA UVUVI**

Alieleza, kwa kutambua kwamba sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi, ndiyo mwajiri mkuu kwa Watanzania wengi kipindi cha miaka minne, serikali ya awamu ya sita imetoa sh. 333,559,000.00 ambapo sh. 189,559,000.00 zimetumika kusambaza miche ya kahawa 588,530 kwa wakulima 1583.

Alisema afya ya mifugo imeimarishwa ambapo sh. 144,000,000.00 zimetumika kutoa chanjo ya dhidi ya magonjwa ya homa ya mapafu, chambavu, homa, mapele na magonjwa mengine nyemelezi, jumla mifugo 51,471 wamepatiwa chanjo na uhamilishaji umefanyika kwa ng'ombe 4019, lengo likiwa ni kufuga kwa tija zaidi.

"Mazingira ya uvuvi yameendelea kuboreshwa kwa kukarabati eneo la kupokelea samaki na eneo la kuegesha mitumbwi katika mwalo wa Kabindi. Jumla ya pikipiki 51 zimetolewa kwa wataalam 51 wa ugani kwa lengo la kuhakikisha wakulima na wafugaji wanafikiwa kwa urahisi,"alisema.



Ujenzi wa shule mpya Bunazi B

**UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI**

Alisema serikali imeendelea kuimarisha sekta binafsi hususan wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kwa lengo la kuzalisha ajira kwa kutumia raslimali zinazopatikana maeneo yao.

Alieleza kuwa, kwa kipindi cha miaka minne serikali imetoa mikopo ya sh. 2,900,954,000.00, kwa vikundi vya wanawake 270 vyenye thamani ya sh. 1,382,379,531.

"Vijana vikundi 146 vyenye thamani ya sh. 1,445,661,969 na watu wenye ulemavu vikundi 32 vyenye thamani ya sh. 72,912,500, hivyo kuzalisha ajira 2,120 3.3,"alisema.

**BARABARA NA MAWASILIANO**

Mkurugenzi Wanga alisema kwa kipindi cha miaka minne ya Rais Dk. Samia, Wilaya ya Missenyi imepokea kiasi cha sh. 5,950,783,689.39, ambapo ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilometa 2.45 zimejengwa kukiwa na ongezeko la kilometa 2.75 za mwaka 2020, kufanya barabara za lami kufikia kilometa 5.2.

Alisema barabara za changarawe zenye kilometa 109.105 zimetengenezwa kukiwa na ongezeko la kilometa 211.43 kwa mwaka 2020, hivyo kufanya barabara za changarawe hadi sasa kufikia kilometa 320.535 makalvati 72 yametengenezwa ambapo kwa sasa Wilaya inapitika kwa majira yote ya mvua na kiangazi.

**MIUNDOMBINU NA HUDUMA YA UMEME KATIKA WILAYA**

Alieleza kuwa, kwa kutambua umuhimu wa Nishati ya Umeme kwa Maendeleo ya Wananchi, Kiwango cha uunganishwaji wa umeme Vijijini (REA) katika Wilaya kimeongezeka kutoka Vijiji 74 kati ya 77 kufikia vijiji 77 sawa na asilimia 100.4.

**UKUSANYAJI WA MAPATO YA NDANI**

Mkurugenzi Wanga alisema kwa kipindi cha miaka minne, ukusanyaji wa mapato umeongezeka kutoka Tsh 3,710,576439.69 kwa mwaka 2020/2021 hadi kufikia Tsh 10,421,365,483.62, Mei 31 kwa mwaka 2024/2025 kutokana na makusanyo haya, Halmashauri imeweza kutoa huduma vizuri na kutekeleza miradi ya kawaida na miradi ya uwekezaji.

**MIRADI YA UWEKEZAJI**

Alisema kwa kipindi cha miaka minne, Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi imetekeleza miradi ya kimkakati yenye thamani ya sh 1,070,000,000.00, miradi hiyo ni uboreshaji wa stendi ya Kyaka ambapo limejengwa jengo la wauza ndizi aina ya gonja, kumwaga kifusi na kushindilia na Ujenzi wa vibanda 17.

"Miradi mingine ni uboreshaji wa soko la Bunazi ambapo mapaa sita yamejengwa. Halmashauri imejenga, maegesho ya malori Mutukula, jengo la abiria, uboreshaji wa mnada Kakunyu. Miradi inayoendelea ni Ujenzi wa soko la Sabasaba Rukurungo, ujenzi wa soko la mazao Bugango na ujenzi wa stendi na gulio Gera," alisema.

Alisema mpango uliopo kwa sasa ni kujenga soko la Bunazi ambapo lipo hatua ya kumtafta Mkandarasi, kujenga meghalaya na viwanda vya kusindika mazao eneo la Kabakesa.

Mkurugenzi Wanga, alimshukuru na kumpongeza Rais Dk. Samia kwa kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo mbalimbali Missenyi.

Alisema mafanikio yaliyoelezwa ni kiashiria tosha kwamba utekelezaji wa Ilani ya CCM, umefanyika kwa kiwango cha juu. mshikamano na uwajibikaji wa viongozi kutoka ngazi ya mkoa, wilaya hadi ngazi ya mamlaka ya msingi umekuwa ni nguzo imara kufikia tulipo.

UHURU

Jumatano Oktoba 15, 2025





# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## MKOA WA KAGERA

# ASANTENI WASHIRIKA

**Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Uhuru Publications Limited, inawashukuru na kuwapongeza kwa kufanikisha uandaaji wa toleo maalumu la mafanikio ya Mkoa wa Kagera.**


Gazeti hili hutolewa na Uhuru Publications Limited, S.L.P. 9221 Dar es Salaam